SUPA JACKPOT
TZS. 1,114,965,687
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Kitendawili** kuwasili mwili wa Mkono chateguliwa

UKURASA 4




UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Mei 21, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
JUMAPILI
ISSN 0856 • No. 0581317
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# NJOZI YATIMIA

• **Ni** serikali kuhamia rasmi Dodoma, Ikulu yazinduliwa, JK asema historia imeandikwa...*Endelea Ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### IGP WAMBURA AAGIZA ASKARI 19 WASHTAKIWE

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, ameagiza askari wanane wasipewe vyeo vya kijeshi, huku akiamuru askari wengine 19 walioachishwa mafunzo...



Jengo la Ikulu ya Chamwino, Dodoma likionekana baada ya kukamilika. **Picha ndogo**: Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa jengo hilo jijini Dodoma jana. Wengine kutoka kushoto ni Wazari Mkuu, Kassim Majaliwa ,Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango. Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, kushoto kwake wa kwanza ni Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi ,Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH. PICHA ZAIDI UK. 2 & 8.**

## Wamiliki wa baa, hoteli wamtikisa RC Makalla

UKURASA 3



UKURASA. 3




## Wazazi wasimulia machungu kuondolewa Toto Afya Kadi

MICHEZO YANGA, SINGIDA BS HAPATOSHI FA CUP UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Rais mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, akizungumza wakati wa sherehe za ufunguzi wa jengo la Ikulu ya Chamwino Jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Njozi yatimia serikali kuhamia Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema uzinduzi wa jengo jipya la Ikulu ya Chamwino ni uthibitisho wa kukamilika kwa adhma ya serikali ya kuifanya Dodoma kuwa makao makuu, kwamba hakuna kurudi nyuma.

Aliyasema hayo jana Chamwino mkoani hapa wakati akizindua jengo hilo katika hafla iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa wakiwamo marais wastaafu wa awamu zilizopita.

"Wale waliokuwa na mashaka ya kutimia kwa shughuli ya kuhamia Dodoma kwa sasa wameamini hakuna kurudi nyuma 'We are here to stay', tupo Dodoma, Dar es salaam tutakwenda kupokea wageni wetu wa kimataifa, tutakwenda kufanya kazi zinazopaswa kufanywa Dar es Salaam.

"Tutakapomaliza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato na nyumba zetu katika awamu ya pili ya ujenzi wa Dodoma hata wageni wa kimataifa tutawapokea hapa hapa Dar es Salaam tunaiacha kuwa mji wa biashara," alisema.

Rais Samia alisema Serikali ya Awamu ya Tano iliyoongozwa na Hayati John Magufuli ilitekeleza azma ya serikali kuhamia Dodoma kwa msukumo zaidi.

"Julai 2016 Hayati Magufuli alikumbusha mkutano mkuu wa CCM kuhusu uamuzi wa kuhamisha shughuli za serikali kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na siku mbili baadaye Siku ya Mashujaa, alisisitiza dhamira yake na baada ya hapo, utekelezaji wa miradi mbalimbali Jiji la Dodoma uliendelea kwa kasi zaidi ikiwa ni pamoja na upanuzi wa Ikulu ya Chamwino.

"Mzee wetu Mwinyi alisema maisha ni hadithi na kututaka tujitahidi kuandika hadithi njema za maisha yetu. Katika utekelezaji wa wazo hili la kuhamishia serikali Dodoma. Hakika Hayati Magufuli ameandika hadithi yake hatutaweza kuandika historia ya shughuli hii bila kuwepo kwa tahariri ya mchango wake mkubwa," alisema.

Samia alisema mchakato wa kuhamishia serikali mkoani Dodoma ulikuwa wa muda mrefu na wa kidemokrasia na ujenzi huo ni wa nguvu za awamu zote za uongozi.

Alisema alipokabidhiwa uongozi aliahidi kuendeleza mema yaliyopo, kuboresha na kuleta mema mapya kwa misingi ya kauli mbiu ya kazi iendelee.

"Ujenzi wa Ikulu ni moja ya miradi niliyorithi kutoka kwa Hayati John Magufuli, mtakumbuka mradi wa kwanza kukamilisha ulikuwa Daraja la Tanzanite huu ni mradi wa pili na inshallah Mungu anipe uwezo niikamilishe yote," alisema.

**SAMIA COMPLEX NDANI YA IKULU**

Rais alisema katika eneo la Ikulu bado kuna kazi za kufanya na hatua inayofuata ni ujenzi wa jengo la kisasa ambalo litaitwa 'Samia Complex' litakalokuwa na ukumbi wa mikutano utakaochukua watu 2,000 hadi 3,000, nyumba za viongozi hasa wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Kutakuwa na Zanzibar Lounge, East Africa Lounge, kutakuwa na uwanja wa gofu, njia ya ndege, viwanja vya michezo mbalimbali, sehemu za historia za viongozi wa nchi yetu, michoro ipo tayari tunahangaika kutafuta fedha ili kuanza ujenzi huo," alisema.

**HISTORIA MAKAO MAKUU**

Rais Samia alisema mwaka 1966 Mbunge wa Musoma, Joseph Nyerere, ambaye alikuwa mdogo wa Hayati Mwalimu Nyerere, aliwasilisha hoja binafsi bungeni akitaka makao makuu ya serikali yahamishiwe Dodoma jambo ambalo lilipingwa, hoja yake kuondolewa.

"Aprili 1972 Kamati ya Utendaji ya TANU ya Mkoa wa Mwanza ilibua tena wazo hili na kuliwasilisha pendekezo rasmi kwa Kamati Kuu ya TANU na kuamua pendekezo hilo lijadiliwe kwenye matawi yote 1,859 ya TANU yaliyokuwepo wakati huo na kufanyiwa uamuzi na matokeo yake matawi 1,017 yaliunga mkono na matawi 842 yalipinga," alisema Rais Samia.

Ilipofika mwaka 1973, alisema Halmashauri Kuu ya TANU ilipitisha azimio kwamba makao makuu ya serikali yahamishiwe Dodoma na kazi hiyo ifanyike katika kipindi cha miaka 10.

"Tangu mwaka 1973 Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alivyoutangazia umma kazi ya kuendeleza mji ilianza na haikuwa rahisi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo za kiuchumi na kuifanya safari hiyo kuwa ndefu zaidi kuliko ilivyopangwa," alisema Rais Samia.

Alisema safari hiyo ilikuwa ndefu kuanzia mwaka 1973 hadi 2023 na imekuwa ya miaka 50 badala ya miaka 10 iliyoagizwa na Halmashauri Kuu ya TANU.

**MAELEKEZO YA SERIKALI**

Akitoa maelezo mafupi ya serikali, Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Moses Kusiluka, alisema uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa jengo hilo ulifanyika Mei 30, 2020 na uliongozwa na Hayati Rais John Magufuli ambaye aliambatana na marais wastaafu.

Alisema Ikulu ya Dar es Salaam ilijengwa na wakoloni na ujenzi wake ulikamilika mwaka 1923, kwamba ni miaka 100 imepita tangu ijengwe.

"Mradi umetekelezwa na Watanzania kwa asilimia 100, ujenzi umefanywa na Jeshi la Kujenga Taifa na Wakala wa Majengo Tanzania alikuwa mshauri elekezi na Ofisi ya Rais nayo ilisimamia kwa karibu sana.

"Ujenzi wa barabara ulisimamiwa na Wakala wa Barabara nchini kwa kiasi kikubwa vifaa vya ujenzi vimezalishwa hapa nchini na samani za jengo hili zimetengenezwa nchini,"alisema.

Alisema kukamilika kwa jengo hilo kunatimiza adhma ya serikali kuhamia Dodoma na Rais Samia alipoingia madarakani ujenzi wa mradi huo ulikuwa umefikia asilimia 70.

# JK: Historia imeandikwa kwa wino wa dhahabu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Mstaafu Jakaya Kikwete amesema ujenzi wa Ikulu ya Chamwino, Dodoma ni historia mpya iliyoandikwa kwa wino wa dhahabu.

Aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipozungumza wakati wa uzinduzi wa Ikulu hiyo kwa niaba ya marais wastaafu.

Pamoja na mambo mengine, Kikwete alisema: "Hili ni jengo ambalo tumejenga wenyewe. Wataalamu wetu walichora, wakasanifu, tumetoa fedha zetu wenyewe kujenga. Leo limekamilika. Tukio hili linahitimisha dhamira ya Baba wa Taifa (Hayati Mwalimu Julius Nyerere) ya kuhamisha makao makuu kutoka Dar es salaam kuleta Dodoma. Uamuzi ulifanyika mwaka 1971 leo (jana) mama yetu (Rais Samia Suluhu Hassan) amekamilisha.

"Maana kilele ni Rais kuhamia Dodoma na si kwa kupita bali kuwa na ofisi yake Dodoma. Sasa katika kila awamu, yapo yaliyofanyika maana uongozi ni kazi ya kupokezana kijiti. Unafanya, anakuja mwenzako anafanya. Anasogeza mbele hadi mnafika mwisho wa safari.

"Yako yaliyofanywa kwa Mwalimu Nyerere, (Ali Hassan) Mwinyi, (Benjamin) Mkapa. Katika kipindi changu uamuzi wa msingi tuliofanya ni kuamua kwamba Ofisi ya Rais na makazi ya Rais yatakuwa hapa Chamwino maana wazo lililokuwapo mwanzoni lilipangwa Chimwaga ndiyo yatakuwa makao makuu ya Chama cha TANU na makao makuu ya serikali," alisema.

"Mimi nilipokuja nikaamua pale tujenge Chuo Kikuu tulikuwa na mjadala. Mawazo yalikuwa mengi lakini tukaamua tujenge Chuo Kikuu cha Dodoma. Baada ya pale kupatumia kwa ajili ya chuo kikuu, tulifanya kikao na CDA (iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao makuu) wakati William Lukuvi akiwa Waziri wa Ardhi.

"Nikawaambia sasa maelekezo yangu kuwa makazi ya Rais yajengwe Chamwino na ofisi za mawaziri zijengwe karibu na hapo kulikuwa na mjadala wakasema Chamwino siyo Dodoma nikawaambia Chamwino ni Dodoma na jambo la kufanya nendeni Malaysia wamejenga makao makuu ya serikali mapya na huko ndiyo kuna makazi ya Waziri Mkuu na Mfalme.

"Wamejenga vizuri unapita ofisi za mawaziri juu kule mwishoni ndiyo ofisi za Rais wamekwenda kuifanya hiyo kazi na ndiyo tunaiona sasa, niliwaambia kwa kuwa Baba wa Taifa alianzia Chamwino tusitoke nje ya hapa," alisema.

Kikwete alisema Rais wa awamu ya tano, Hayati John Magufuli, alitoa msukumo mkubwa wa ujenzi wa wizara za serikali na akaanza safari ya ujenzi wa Ikulu ya Chamwino.

Kadhalika, alimpongeza Rais Samia kwa uongozi wake na wale waliofanya kazi kubwa ya ujenzi wa Ikulu hiyo kwa kuwa wameliheshimisha taifa.

"Rais unafanya kazi nzuri sana, mwenye macho haambiwi tazama. Umepokea miradi mingi mikubwa ya gharama kubwa. Ungeweza kusema aah! naanza na yangu lakini hukufanya hivyo. Umesema kila kilichoanzwa na mtangulizi wangu tutakimaliza pamoja na mzigo mkubwa uliokuwapo kazi inaendelea.

"Sote tunaona inavyokwenda labda tu kama mtu ana roho mbaya ni kukuombea Rais wetu umri mrefu, afya njema ili uweze kuwa na maono yaliyo makubwa kuliko yalivyo hivi sasa,"alisema.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema ujenzi huo ni lulu ya Tanzania na jingo hilo lina hadhi ya nchi yenye kipato cha kati.

"Hii ni taa ya kuipeleka nchi yetu yenye hadhi ya kipato cha juu ndani ya kipindi kifupi. Nakupongeza Rais kwa kazi nzuri ya kuongoza taifa letu kwa kuhakikisha tunapata maendeleo na kutunza amani,"alisema Dk. Mpango na kuongeza kuwa Ikulu hiyo ni kazi ya vichwa na kodi za Watanzania.

"Watumishi wa Ikulu jengo lile liheshimiwe na litunzwe vizuri na litumike kwa ajili ya kutoa maamuzi na kumsaidia Rais kuamua hatma ya Tanzania tunavyokwenda mbele," alisisitiza.

## HABARI KITAIFA

# Wazazi wasimulia machungu kuondolewa Toto Afya Kadi

**Na Christina Mwakangale**

ZIKIWA zimepita takribani siku 60 tangu kusitishwa kwa usajili mpya huduma ya 'Toto Afya Kadi' maalumu kwa ajili ya watoto, baadhi ya wazazi na walezi wenye watoto wameeleza magumu wanayopitia kutokana na gharama kubwa wanazolipia kupata huduma.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ulitangaza kwamba utaratibu wa malipo ya Sh. 50,400 ya huduma ya 'Toto Afya Kadi' umeondolewa kuanzia Machi 13, mwaka huu, kwa ambao bima zao zimekwisha na wanaohitaji wajiunge kwa mfumo mpya.

Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inasema huduma za afya kwa wazee, wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, huduma za matibabu ni bure. Uchunguzi uliofanywa na Nipashe kwa kipindi hicho, ulibaini kwamba watoto walio chini ya umri huo, hususan wanaougua magonjwa sugu yakiwamo ya moyo, himofilia na kifafa, hulazimika kulipia Sh. 30,000 hadi 130,000 kwa kila kliniki kwa mwezi, kutegemeana na hospitali.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, Brenda Milton, mzazi wa Francis Maringo mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu, alisema mtoto wake anaugua pumu na mara kadhaa huugua na kuhitajika kufikishwa hospitalini kwa ajili ya matibabu.

"Mara ya kwanza sikufahamu kama ana tatizo hilo ila nilikuwa naona anasumbuliwa na kifua kumbana kila mara, uchunguzi ukabaini ana pumu. Mara ya mwisho aliumwa wakati bima yake haijaisha lakini sasa tangu huduma ya kusajili tena kuisha ni bima imkesha nalipia fedha taslimu.

"Mbali na gharama za dawa alipoumwa Aprili, mwaka huu, alilazwa kwa siku tatu katika hospitali maarufu (jina tunalo) iliyoko Gongo la Mboto. Nililipa Sh. 286,000 kwa siku hizo, hapo bado dawa," alisema Milton.

Latifa Mathayo, mkazi wa Kinondoni, Dar es Salaam, alisema alijiunga na huduma za mfuko huo mwaka 2019 kwa kumlipia mwanawe bima kwa Sh. 50,400 kwa mwaka, akihitajika kufanya malipo hayo kila mwaka.

"Mwanangu aligundulika kuwa ana matatizo kwenye ubongo baada ya kuugua ugonjwa wa kifafa na kuhitajika kuhudhuria kliniki Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kila mwezi. Sasa bima yake imekwisha Machi, mwaka huu, hivyo ninalipia huduma hiyo kwa fedha taslimu," alisema.

"Kila mwezi nahudhuria kliniki ya watoto MNH na kila siku anatakiwa kumeza dawa. Kumuona daktari bingwa ni Sh. 30,000 na ipo aina moja ya dawa dozi yake siku 30 jumla Sh. 60,000 na aina nyingine anapewa kidonge kimoja anatumia kwa siku mbili namkatia nusu kinauzwa Sh. 15,000.

"Kila mwezi natakiwa niwe na Sh. 150,000 au 200,000 kwa sababu kuna wakati mwingine dawa alizoandikiwa hazipo Muhimbili, nanunua kwenye maduka ya nje bei ni juu zaidi. Ninafanya kazi yenye mshahara wa Sh. 250,000 kwa mwezi," aliongeza.

Naye Aloysia Mosha, mkazi wa Makumbusho, Dar es Salaam, alisema mtoto wake anaugua ugonjwa wa moyo na kila mwezi anahudhuria kliniki ya watoto wenye ugonjwa huo, Hospitali ya Dar Group ambayo ni tawi la Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

"Daktari bingwa kumwona kila mwezi ni Sh. 130,000 kama huna bima japokuwa serikali inasema matibabu ya watoto chini ya miaka mitano huduma za matibabu ni bure. Kiukweli hilo halipo au kama zipo si dawa zote utapata, hivyo mzazi inabidi nitafute pesa," alisema.

Regina Valence, Mwenyekiti wa Wanawake wa Chama cha Himofilia Tanzania, na mzazi wa watoto wawili wanaougua ugonjwa wa himofilia, alisema umoja huo wenye wanachama wanaokadiriwa kufikia 200, watoto walio wengi hawana huduma ya bima afya.

"Watoto wetu wao wana kliniki muda wowote akivuja tu damu. Mbali na dawa wanazotumia kila siku, pia huchoma sindano. Wengi wetu hatuna bima, tunaomba ufadhili au serikali iruhusu bima maalum za watoto hawa wenye magonjwa yanayohitaji kliniki za kibingwa na wengi wetu tuna vipato duni na utakuta familia moja ina watoto wawili wana matatizo haya," alisema.

**WADAU WANENA**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) baada ya huduma kwa usajili mpya kwa watoto kuanzishwa kwenye taarifa yake, kilisema Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009 imekiukwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema huduma ya kifurushi maalum cha Toto Afya Kadi ilikuwa msaada kwa watoto hususan wenye uwezo mdogo na kwamba ni kinyume na Sheria ya Mtoto pamoja na marekebisho yake mwaka 2019, Ibara ya 24 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto ya Mwaka 1989 na Ibara ya 14 ya Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto.



Mafundi wa Kampuni ya Ujenzi ya Yapi Merkezi, wakitumia mitambo kumwaga zege katika ujenzi wa daraja eneo la Chang'ombe jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wamiliki baa, hoteli wamtikisa RC Makalla

**Na Vitus Audax,** MWANZA

NI mgomo mwingine unamnyemelea Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, baada ya ule wa Dar es Salaam uliowahusisha wafanyabiashara wa Kariakoo kuhusu kero mbalimbali walizokuwa wakikumbana nazo.

Mgomo huo ulitikisa mapato ya serikali kutokana na eneo la Kariakoo kuwa kitovu cha biashara, baadhi ya watu wanadai kuwa ndio uliomwondoa na kuhamishiwa Mwanza.

Safari hii, wamiliki wa hoteli, baa na kumbi za starehe jijini Mwanza wametishia kufanya mgomo leo kwa kufunga biashara zao. Wafanyabiashara hao wakishinikiza kuondolewa kwa faini na masharti magumu yaliyowekwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Masharti wanayolalamikia ni kuacha kupiga muziki uliopita vipimo, kulipia faini ya Sh.milioni tano pamoja na kununua kipima sauti kinachoelezwa kutokuwa na usahihi katika upimaji wake.

Endapo wafanyabiashara hao wakitimiza adhma hiyo, utakuwa ni mtihani wa pili anakutana nao Mkuu wa Mkoa huo, Amos Makalla katika kipindi cha wiki mbili, wa kwanza alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam dhidi ya wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo.

Walitoa tamko hilo jana walipofanya kikao cha pamoja kujadili hatma ya shughuli zao baada ya kufungiwa kufanya wakitakiwa kulipia faini.

Joseph Gaspati, mmiliki wa hoteli ya Bundasliga alisema maofisa wa NEMC walichukua uamuzi wa kuwafungia huduma za muziki sambamba na kumweka mahabusu bila kupewa elimu yoyote juu ya vidhibiti sauti hivyo.

Alisema pia alitaliwa kulipa faini ya Sh. milioni tano kwa mkupuo ndani ya muda mfupi.

"Huo ni unyanyasaji. Kama hawataki tufanye biashara waseme tufunge hoteli zetu na faini hizo hatulipi. Pia ikifika Jumatatu (kesho) hatujafunguliwa shughuli zetu, tunafunga na watajua watakakopata mapato," alisema

Ester John, mmiliki wa The Femurs Lounge, alisema utaratibu walioutumia NEMC haukuwa wa kistaarabu kutokana na kuwa wakati wa kuanzisha biashara hizo hakuna sehemu walipoelekezwa kuwa wanatakiwa kufika kwenye baraza kupewa sheria na taratibu juu ya upigaji muziki.

"Wengine uwezo wa kulipa faini kwa mkupuo hatuwezi kabisa na hili suala limekuja ghafla maana kama ni sheria na taratibu tulifuta zote lakini hatujawahi kuambiwa kuna utaratibu huu na licha ya hivyo tungeitwa kwanza tupewe elimu ndipo tuanze kutekeleza matakwa yao," alisema.

Aidha, walisema ushirikiano kwa baadhi ya viongozi wa NEMC hauridhishi kutokana na kupewa majibu ya mkato, huku kauli yao ikiwa kutakiwa kulipia faini na kununua kifaa cha kupima sauti.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Mkoa wa Mwanza, Patrick Msagati, aliwaomba wafanyabiashara hao wavumilivu kwa kipindi cha siku mbili wakati yeye na viongozi wenzake wakiendelea kufuatilia suala hilo.


## KUPOTELEWA NA CHETI



**WAKURU LEAH JUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S.3526/0049** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **HUNYARI SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **GEI/CHA/RB/1422697/2023.**

# Kitendawili chateguliwa kuwasili mwili wa Mkono

**Na Sabato Kasika**

MWILI wa aliyekuwa Mbunge wa Butiama mkoani Mara, Nimrod Mkono unatarajiwa kurejeshwa nchini Mei 27 mwaka huu kwa ajili ya mazishi yatakayofanyika kijijini kwao Kigori, Busegwe mkoani Mara.


Mkono aliyekuwa akitibiwa nchini Marekani tangu mwaka 2018, alifikwa na mauti Aprili 18, mwaka huu. Aliondoka kwenda Marekani wakati bado ni Mbunge wa Butiama na jimbo lilibaki wazi hadi ulipofanyika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Kamati ya Kuratibu mazishi hayo, Stephen Wasira, alisema mwili wa Mkono utapokewa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na kupelekwa nyumbani kwake, Masaki, Dar es Salaam.

Wasira ambaye aliwahi kuwa mbunge wa Bunda, alisema: "Mazishi ya Wakili Mkono yanatarajiwa kufanyika nyumbani kwake, kijijini Kigori, wilaya ya Butiama mkoani Mara."

Alifafanua kuwa ratiba kamili ya shughuli zote za kupokea, kuaga hadi kusafirisha mwili kwenda kijijini Kigori itatolewa baadaye.

"Familia inawashukuru ndugu, jamaa, marafiki na serikali kwa kuwa pamoja kwa muda wote huu mgumu wa msiba. Kamati inaomba ndugu, jamaa na marafiki waendelee kushirikiana nayo kwa hali na mali ili kuupokea mwili na baadaye kuupumzisha," alisema Wasira.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Ummy Nderiananga (kulia), akimkabidhi zawadi maalum Rais mstaafu Jakaya Kikwete kwa kutambua mchango wake katika kampeni ya GGML Kili Challenge ambayo ilianzishwa na Kampuni ya GGML mwaka 2002 kwa kushirikiana na TACAIDS kwa lengo la kutokomeza VVU/UKIMWI. **PICHA: GGM**

# IGP Wambura aagiza askari 19 washtakiwe

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, ameagiza askari wanane wasipewe vyeo vya kijeshi, huku akiamuru askari wengine 19 walioachishwa mafunzo baada ya kukutwa na makosa ya utovu wa nidhamu, washtakiwe na adhabu stahiki zitolewe kwa mujibu wa sheria.

Alitoa maagizo hayo jana katika Kambi ya Kambapori iliyoko West Kilimanjaro, wilaya ya Siha, wakati wa kufunga mafunzo ya uongozi mdogo jeshini, ngazi ya sajini meja na koplo, iliyowajumuisha zaidi ya askari 2,200.

Mafunzo hayo ya miezi mitatu yalianza Februari 13, mwaka huu, na yalifikia ukomo juzi.

IGP Wambura aliwakilishwa na Mkuu wa Utawala na Rasilimali Watu katika jeshi hilo, Kamishna (CP) Susan Kaganda.

"Nimepokea ombi hilo la Mkuu wa Shule ya Polisi Tanzania (TPS) na ninawapa fursa ya kurudia mitihani wanafunzi 11 waliokosa kufikia ufaulu masomo ya darasani lakini wana sifa za uongozi.

"Nimeridhia kwamba ndani ya wiki moja, wanafunzi hao 11 wapewe mitihani na ninawakumbusha walimu kwa yeyote ambaye hatafanya vizuri, basi asipewe cheo.

"Pia naelekeza kwa wale wanafunzi watatu, ombi la kutowapa cheo wamefeli na hawana sifa za uongozi. Sambamba na wanafunzi watano waliofaulu, lakini hawana sifa za uongozi, naridhia wasipewe cheo na wale wenye vitendo vya utovu wa nidhamu, washtakiwe na adhabu stahiki kwa mujibu wa sheria zitolewe," alisema.

Katika maelekezo yake, IGP Wambura aliwakumbusha wapiganaji hao uongozi mdogo kwamba ndiyo mwanzo wa kuwa viongozi wakubwa.

Kabla ya kutolewa amri ya IGP Wambura, Mkuu wa Shule ya Polisi Tanzania (TPS), Kamishna Mwandamizi Msaidizi (SACP) Ramadhan Mungi, alimweleza Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kaspar Mmuya, kwamba mafunzo ya sajini meja yalikuwa na wanafunzi 24 na wanafunzi 19 kati ya hao ni wanaume na wanne ni wanawake lakini waliohitimu ni 23.

Aidha, alimweleza katika kozi ya koplo kuwa askari 2, 359 wenye vyeo vya konstebo waliteuliwa na makao makuu ya Jeshi la Polisi kwenda kujifunza mafunzo ya uongozi mdogo ngazi ya koplo lakini askari wanafunzi 140 hawakufika kambini kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema kambi hiyo ilikuwa na zaidi ya wanafunzi 2,200 na ambapo kati yao wanaume walikuwa 1,568 na wanawake ni 632.

"Mheshimiwa Katibu Mkuu (Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi), wanafunzi 19 wa mafunzo haya wameachishwa mafunzo kwa sababu ya utovu wa nidhamu," alisema SACP Mungi.

Akifunga mafunzo hayo, Katibu Mkuu Mmuya aliagiza Mkuu wa Shule ya Polisi Tanzania, kupeleka wizarani taarifa rasmi kuhusu hatua zilizochukuliwa dhidi ya askari waliokutwa na makosa ya utovu wa nidhamu.

"Bila nidhamu, hakuna jeshi. Ni lazima kuwa na nidhamu katika utendaji, kwa sababu huwezi kutekekeza sheria za nchi bila nidhamu. Ninawasihi mkatekeleze majukumu yenu kwa kuviishi viapo vyenu," alisema.

# Bil.1.8/- zatengwa mapambano ukimwi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 1.8 zitakazotumika kuunga mkono jitihada za wadau katika kutunisha Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti Ukimwi (ATF) pamoja na kuendeleza mapambano dhidi ya virusi Vya Ukimwi (VVU).

Hayo yalibainishwa jana Dar es Salaam na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Ummy Nderiananga, wakati wa hafla ya uzinduzi wa harambee ya kampeni ya GGML Kili Challenge inayolenga kuunga mkono juhudi za serikali kukabiliana na janga hilo.

Alisema mbali na kuimarisha upatikanaji wa afua mbalimbali, pia serikali imetenga kiwango hicho cha fedha ili kuungana na wadau wanaoendeleza mapambano dhidi ya VVU.

Katika uzinduzi wa harambee hiyo iliyoongozwa na Rais Mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, Sh. bilioni 1.6 zilipatikana huku lengo la kampeni hiyo ni kukusanya Sh. bilioni 2.3.

Kampeni hiyo iliyoasisiwa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), ilianzishwa mwaka 2002 na kufikia makundi mbalimbali yaliyo katika maeneo hatarishi kwenye janga hilo.

Wakati wa harambee hiyo, Dk. Kikwete alizipongeza GGML na TACAIDS kwa ushirikiano walioufanya na kuanzisha kampeni hiyo. Dk. Kikwete alisema serikali haiwezi kutokomeza janga la Ukimwi bila kuwapo kwa ushirikiano na sekta binafsi. "Hamasa inatakiwa kuendelea kutolewa kwa ukubwa kwa sababu tumetoka mbali, tumepunguza vifo vitokanavyo na ukimwi kutoka 72,000 mwaka 2016 hadi 54,000 mwaka 2021," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong, alisema wakiwa wadau wa mapambano hayo, wamepokea msaada ambao uliiwezesha kampeni hiyo kupiga hatua kubwa hadi kufikia kuwa mfuko wa kimataifa.

Makamu Rais wa AngloGold Ashanti- GGML anayeshughulikia miradi endelevu Ghana na Tanzania, Simon Shayo, alisema tangu kuanzishwa kwa kampeni hiyo, makundi mbalimbali yamefaidika ikiwamo kuazishwa kwa kituo cha kulea watoto yatima na wanaoshi katika mazingira magumu kitwacho Moyo wa Huruma kilichopo Geita.

Alisema katika kundi la kwanza la watoto waliolelewa kwenye kituo hicho sasa wamefikia elimu ya chuo kikuu ikiwamo wawili ambao wanasomea udaktari. Alisema pia wameanzisha vituo vya maarifa katika maeneo hatarishi kwa maambukizi ya VVU, Manyoni na Segera ambavyo vinatoa elimu ya ugonjwa huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alisema fedha zinazokusanywa hupelekwa katika taasisi binafsi zinazoendeleza mapambano dhidi ya ukimwi.

Katika harambee hiyo GGML walitoa Dola za Marekani 500,000.

HABARI KITAIFA

# Mwinyi aahidi ushirikiano mzuri NGO

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali iko tayari kushirikiana na asasi za kiraia kwa sababu zina mchango mkubwa katika kuharakisha mageuzi ya maendeleo ya uchumi wa nchi.

Aliyasema hayo jana mjini Zanzibar katika mkutano wa pili wa jukwaa la asasi za kiraia, hotuba yake ilisomwa na Waziri wa Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo, Shamata Shaame Khamis.

Dk. Mwinyi alisema mchango wa asasi za kiraia kwa kiasi kikubwa umeleta mageuzi makubwa katika kufikiwa kwa huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo sekta ya elimu, afya, maji safi na salama. Alisema wakati asasi za kiraia zikitekeleza majukumu yake kwa ufanisi hazina budi kuweka uwazi wao katika utendaji wa majukumu yao kwa kufuata sheria na kanuni zake.

Dk. Mwinyi alisema migogoro na mivutano katika asasi za kiraia haina nafasi tena, kwamba sheria bora zinazoongoza asasi za kiraia zinahitajika ili kuzifanya asasi hizo kutekeleza majukumu yake.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumejipanga vizuri kufanya kazi na asasi za kiraia katika kuharakisha maendeleo na ujenzi wa taifa kwa sababu mchango wake ni mkubwa, hivyo kwa upande wa asasi nazo zinatakiwa kwenda na wakati na mabadiliko yaliyopo sasa ikiwemo ya sheria."alisema.

Mratibu wa Umoja wa Mataifa Zanzibar, Dorothy Temu, alisema wataendelea kuziunga mkono asasi za kiraia katika kuyafikia malengo yake ambayo yametajwa katika mpango wa malengo endelevu ya dunia.

Alisema malengo endelevu ya dunia yatafikiwa kama asasi za kiraia zitafanya kazi zake vizuri, kuyafikia makundi mbalimbali hadi vijijini katika sekta mbalimbali muhimu za kijamii.

Mrajis wa asasi zisizokuwa za kiserikali, Ahmed Khalid Abdalla, alizitaka asasi hizo kujikita na kufanya kazi zake vijijini ili kuyafikia matatizo yanayowakabili wananchi.

Katibu Mtendaji wa Jukwaa la Asasi za Kiraia, Hassan Khamis Juma, alisema mkutano huo wa mwaka miongoni mwa majukumu yake makubwa ni kufanya tathmini ya kazi za asasi za kiraia pamoja na matatizo yanayowakabili.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis alitembelea mabanda ya maonyesho ya asasi za kiraia ikiwemo zinazojishughulisha na maendeleo ya kilimo na utafiti.



Mwendesha Baiskeli ya miguu mitatu (Guta), akiwa amepakia vipande vya boksi akipeleka kuuza kwa wafanyabiashara wa samaki katika Soko la Kimataifa, Feri jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DART kusafirisha abiria milioni tatu 2030

**Na Joseph Mwendapole,**
DODOMA

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), umesema utakuwa na uwezo wa kusafirisha abiria 3,000,000 kwa siku baada ya kukamilika kwa ujenzi wa awamu zote sita ifikapo mwaka 2030.

Umesema kukamilika awamu hizo kutasababisha ajira kwa madereva 7,569 ambao watapewa mafunzo, mabasi kwenye mradi huo yatakua 3,290.

Meneja Mipango na Usafirishaji wa DART, Mhandisi Mohamed Kuganda, alisema hayo hivi karibuni wakati akiwasilisha mada kuhusu uendeshaji na upangaji wa mabasi kwenye semina ya waandishi wa habari inayoendelea mkoani Dodoma.

Alisema kwa sasa mradi huo unasafirisha abiria 200,000 kwa siku lakini ujenzi wa awamu zote za miundombinu unaoendelea, utawaongezea uwezo mkubwa wa kusafirisha abiria na kuwa nchi ya mfano Afrika kwa miundombinu bora ya usafiri.

Alisema Tanzania itakuwa ya pili baada ya Colombia ambayo kwa sasa ina uwezo wa kusafirisha abiria 3,000,000 kwa siku kwa mabasi hayo yaendayo haraka.

Kuganda alisema hali hiyo itaiwezesha Tanzania kupunguza uchafuzi wa hewa na kupata sifa kimataifa kwani matumizi ya mabasi hayo yatapunguza kwa kiwango kikubwa matumizi ya usafiri binafsi. Alisema awamu ya kwanza ya mradi wa miundombinu ya mabasi hayo ilianza njia ya Kivukoni kwenda Kimara wakati awamu ya pili imeanzia Kivukoni kwenda Mbagala.

Kuganda alisema ujenzi wa mradi huo kwa sasa umefikia asilimia 90 na unatarajiwa kukamilika Desemba, mwaka huu. Alitaja awamu ya tatu ni kuanzia Kivukoni kwenda Gongo la Mboto ambao ujenzi wake kwa sasa umefikia asilimia 10 na utakamilika Agosti 2024 na awamu ya nne itaanzia Tegeta DAWASA hadi Kivukoni.

Meneja huyo alisema awamu ya tano itahusisha njia ya Ubungo Barabara ya Mandela kwenda Daraja la Mwalimu Nyerere Kigamboni na ujenzi wake unatarajiwa kuanza mwaka huu na kukamilika mwaka 2025.

Alisema wakati awamu ya sita itakuwa na vipande vitatu vya ujenzi wa njia hizo na itahusisha barabara za Mwai Kibaki, kuongeza kipande cha Morogoro (kutoka Kimara hadi Kibaha) na kuongeza kipande cha Kilwa (kutoka Mbagala Rangi Tatu hadi Vikindu).

Kuganda alisema wazo la kutekeleza BRT liliibuliwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam mwaka 2002 ikiwa ni moja ya hatua muhimu za kuboresha usafiri wa umma katika Jiji la Dar es Salaam.

# Singida yaingiza bil.1/- uzalishaji asali na nta

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKOA wa Singida umeingiza Sh.bilioni 1.030 katika sekta ya ufugaji nyuki zilizotokana na uzalishaji wa asali tani 89 na nta katika kipindi cha mwaka 2017 hadi 2022.

Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, aliyasema hayo jana katika hotuba iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskas Mragili, wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Kitaraka Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni.

Mragili alikuwa geni rasmi wakati wa utundikaji mizinga ikiwa ni uzinduzi wa maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani yanayofanyika kitaifa mkoani hapa.

Alisema katika kipindi hicho uuzaji asali umeuingizia Mkoa wa Singida Sh.milioni 890 na nta Sh.milioni 150 na pia kumekuwa na ongezeko la wafugaji wa nyuki kutoka 5,675 mwaka 2017/2018 hadi kufikia wafugaji nyuki 12,133 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 113.8. Serukamba alisema katika kipindi hicho pia kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa asali kutoka tani 58 mwaka 2017 hadi kufikia tani 89 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 53.4 uzalishaji wa nta kutoka tani 13 hadi kufikia tani 30 ambalo ni ongezeko la asilimia 53.85.

Alisema pamoja na mafanikio hayo kumekuwa na matatizo ambayo yanatishia uendelevu wa sekta ya nyuki ambazo ni pamoja na matumizi ya dawa za kuua wadudu kwenye kilimo, uchomaji moto misitu na kubadilisha maeneo ya ardhi ya misitu kwa ajili matumizi mengine.

Tatizo lingine ni kuongezeka kwa kasi ya mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo yanaambatana na mabadiliko ya hewa na mazingira rafiki kwa nyuki kuzalisha mazao yao. Serukamba alisema pamoja na matatizo hayo Mkoa wa Singida bado una nafasi kubwa ya kukuza na kuendelezwa sekta ya nyuki kwa kuhakikisha misitu katika ardhi za vijiji, misitu ya halmashauri, misitu ya serikali kuu na hifadhi za wanyampori inalindwa.

Ofisa Misitu Mkoa wa Singida, Charles Kidula, alisema wananchi wa Kijiji Cha Kitaraka na vijiji jirani wanatumia uoto wa vichaka vya Itigi kufanya shughuli za ufugaji nyuki, kuna vikundi vitatu vyenye wanachama 52.

Alisema vikundi hivyo vya ufugaji nyuki ambayo ni ukombozi, nguvumali na wachapakazi, vina mizinga ya kienyeji 100 na ya kisiasa 27.

Meneja Mradi wa BEVAC, Martin Mgallah, unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) alisema katika maadhimisho hayo wametoa mizinga 50 kwa vikundi 10 vinavyojishughulisha na ufugaji nyuki katika Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni.z

Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki, Deusidedit Bwoya, alisema maadhimisho hayo yanakwenda sanjari na utundikaji wa mizinga ikiwa ni ishara ya kuendelea kuhamasisha jamii kushiriki kwenye ufugaji wa nyuki kibiashara.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Benki zifanyie kazi maagizo ya serikali

**MAKAMU** wa Rais, Dk. Philip Mpango, juzi alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa semina ya wanahisa wa Benki ya CRDB na wadau wengine jijini Arusha na kutoa maagizo kwa benki na taasisi za fedha nchini ikiwamo kufanya kila liwezekanalo kuhakikisha hazizalishi mikopo mipya chechefu.

Hatua hiyo ya Dk. Mpango ambaye kitaaluma ni mchumi mbobezi, alisema itawezesha benki na taasisi za fedha zinazofanya shughuli hiyo kibiashara, kuwa na uhakika zaidi wa uwekezaji katika sekta ya fedha.

Sambamba na agizo hilo, pia alizitaka benki za biashara ziendelee kuzingatia ufanisi katika utendaji, ikiwamo kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Katika mkakati wa kupunguza mikopo chechefu, alisema ni muhimu menejimenti za benki zihakikishe hakuna mikopo chechefu mipya na kuzingatia ukomo wa asilimia tano uliowekwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Pamoja na kuweka wazi mambo hayo, kwa mujibu wa kiongozi huyo, bado kuna changamoto kubwa katika sekta hiyo ambazo zinapaswa kupatiwa ufumbuzi. Moja ya changamoto hizo, ni baadhi ya Watanzania hasa wanaoishi vijijini kutofikiwa au kutotumia huduma za fedha huku akibainisha kuwa ni asilimia 8.6 tu ya wananchi wanaoishi maeneo hayo ndio wanaopata huduma za benki kwa sasa.

Pia alisema kikwazo kingine katika sekta hiyo ni masharti magumu na riba kubwa za mikopo hali inayofanya watu wengi kutonufaika na huduma za mikopo hivyo kushindwa kujikwamua katika umaskini.

Ni dhahiri kwamba sekta ya fedha hususan tasnia ya kibenki ni nguzo muhimu katika ukuaji wa uchumi kwa kuwa ni moja ya vyanzo ambavyo vinaweza kutoa fedha kwa wafanyabiashara na wawekezaji katika kuanzisha miradi na kukuza shughuli zao. Pamoja na umuhimu huo, tasnia hiyo kwa kiasi kikubwa imekuwa kikwazo katika kutimiza azma hiyo.

Ni Watanzania wachache ambao hawafiki hata asilimia 25 wanaoweza kupata huduma za mikopo katika benki hapa nchini sababu kubwa zikiwa ni masharti magumu yanayowekwa na taasisi hizo. Miongoni mwa masharti hayo ni kuwa na dhamana hasa mali isiyohamishika kwa wale wanaotaka mikopo mikubwa ya kuendesha biashara.

Hali hiyo pia imeibuka hata kwa taasisi ndogo za fedha zinazotoa mikopo ya muda mfupi kwamba mtu akitaka mkopo hata wa Sh. milioni moja ni lazima awe na dhamana. Kwa ujumla, jambo hilo linasababisha ukuaji wa uchumi na mpango wa kupunguza umaskini miongoni mwa Watanzania kuwa mgumu.


Kutokana na ushauri uliotolewa na Makamu wa Rais, ni wakati mwafaka sasa kwa benki na taasisi za fedha chini ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), zikaandaa sera za ukopeshaji ambazo ni rafiki kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania wengi kupata huduma hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa itachochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

Kuwapo kwa sera na unafuu wa mikopo, kwa maneno mengine, kutawazesha wafanyabiashara wakubwa ambao wana miradi ya kimaendeleo kama vile viwanda na biashara, kupata fedha ambazo zitawezesha kupanua biashara zao na vitegauchumi na hatimaye kutoa ajira kwa vijana wengi ambao hasa wanahangaika mitaani wakitafuta kazi.

Wakati umefika sasa kwa taasisi zetu kufikiria zaidi katika kushiriki kukuza uchumi wa nchi kwa kuwezesha wafanyabiashara na wawekezaji kupata mikopo kwa ajili ya miradi ya kiuchumi na kijamii ambayo itakuwa kichocheo kikubwa katika maendeleo ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hongera Rais Samia, endelea kuongeza mishahara kimya kimya

Na Sabato Kasika

**KAMA** ilivyozoeleka kwa baadhi ya wafanyabiashara, huwa wanapandisha bei ya bidhaa mara tu wanaposikia serikali imeongeza mshahara na marupurupu kwa wafanyakazi kila mwaka.

Uviziaji huo hufanyika wakati wa Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), kwani wafanyabiashara walishajua kuwa hicho ndicho kipindi ambacho serikali huwa inatangaza nyongeza hiyo.

Mtindo huo kwa namna moja au nyingine, umekuwa ukichangia kuumiza watumishi na watu wengine hasa wa hali ya chini, kutokana na ukweli kwamba wengi wao ni maisha ya kawaida, kwa maana ya kipato kidogo.

Pamoja na hayo, fedha ndio kila kitu katika maisha ya dunia hii, lakini pia mtindo wa baadhi ya wafanyabiashara kupandisha bei ya bidhaa bila kuangalia kundi lingine la watu wenye hali ya chini, unaumiza.

Hata hivyo, serikali imeshtukia janja yao na sasa imeamua kuja na utaratibu mpya ambao utatumika kuongeza mishahara ya wafanyakazi au watumishi wa umma bila wafanyabiashara hao kujua.

Lengo la utaratibu mpya ambao serikali imebuni, ni kutaka kukabiliana na mtindo wa kuvizia nyongeza za mshahara na kupandisha bei ya vitu, kwa madai kwamba mishahara imekuwa mikubwa.

Huo ni utaratibu uliotangazwa na Rais Samia, katika maadhimisho ya Sikukuu ya Wafanyakazi Mei Mosi, ambayo kitaifa mwaka huu ilifanyika mjini Morogoro hivi karibuni.

Tofauti na jinsi ambavyo watumishi wamezoea kutangaziwa nyongeza ya mshahara wakati wa sikukuu hiyo, safari hii Rais anasema sasa utaratibu huo umewekwa pembeni, badala yake wanaongezewa kimya kimya.

Katika ufafanuzi wake, Rais Samia anasema serikali yake itakuwa inaongeza mshahara kila mwaka na kulipa malimbikizo katika kipindi cha bajeti ya mwaka wa fedha ujao.

Anaongeza kuwa si rahisi wafanyabiashara wanaovizia atangaze mshahara mpya, ili wapandishe bei ya bidhaa kushindwa kujua kinachoendelea na hivyo wateja kupata bidhaa kwa bei ya kawaida.

Kwa msemo wa mitaani, ni kwamba wafanyabiashara waliozoea mtindo huo unaoumiza watu wote hasa wa hali ya chini, 'imekula kwao', kwani ni wazi utaratibu huo mpya hauwapi mwanya kujua kinachoendelea.

Ninaamini kwamba hata wale wamilikii wa nyumba za kupangisha nao itakuwa imekula kwao, kwani hao nao huwa ni wepesi kuwapandishia kodi wapangaji wao mara tu wanaposikia mishahara mipya.

Wote kwa pamoja wakiwamo wafanyabiashara, huwa wana vizia maeneo mawili, Mei mosi au mwanzo wa mwaka wa serikali ambao ni Julai ambapo hupandisha bei za bidhaa au kodi za pango. Lakini kwa mfumo ambao Rais amekuja nao, ninaamini unaweza kuwa na mchango mkubwa, katika kuwapunguzia wananchi makali ya maisha ambao wamekuwa wakikumbana nayo.

Kitendo cha kuwapa nyongeza ya asilimia 23 wafanyakazi wenye mishahara ya chini bila kutangaza, ni dalili tosha kwamba ameamua kufanya mambo yake kimya, kimya.

Hatua hiyo inaonyesha jinsi alivyodhamiria kuboresha maisha ya Watanzania, kwani tangu akabidhiwe usukani wa kuongoza nchi, daima amekuwa akibuni mbinu mbalimbali za kutimiza lengo hilo.

## FIKRA MBADALA

# Wosia wa Le Mutuz kwa CCM, wapinzani, serikali uzingatiwe



Pascal Mayalla

WIKI iliyopita kwenye safu hii niliandika Buriani ya Benard Membe na Wiki hii ni buriani nyingine. Hii ni buriani ya mtu wa kawaida tu ambaye si kiongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wala si kiongozi wa serikali.

Ni mtu wa kawaida aliyefahamika na wengi, hivyo maneno ya mtu wa wengi ni maneno ya wengi na sauti ya wengi ni sauti ya Mungu. Hii ni makala ya kuitaka CCM, serikali na wapinzani kuzingatia sana wosia wa mtu huyu.

Huyu ni William Malecela, ambaye anajulikana sana kwa jina maarufu la Le Mutuz kutokana na kuendesha ukurasa wake wa Le Mutuz Super Brand kwenye mitandao ya kijamii. Kuna wengi wanaomfahamu zaidi William kutokana na umaarufu wake kwenye mitandao ya kijamii kama Le Mutuz, hivyo sifa zake kama William Malecela, kujikuta zimeishia Jamii Forums pekee. William Malecela alifariki dunia ghafla wiki iyopita na kuzikwa kijijini kwao, Mvumi mkoani Dodoma Jumatano iliyopita.

Wosia ni maneno ya mwisho ya mtu anayoyaacha kuzungumzia jambo Fulani. Wosia huo unaweza kuwa wa maneno ya kuambiwa au kuandikwa. Wosia wa William Malecela kwa CCM na serikali, ni wa maneno ya kuzungumza. Alisema bila kupanga na tulikutana tuu viwanja vya Sabasaba, nikamfanyia mahojiano. Kwa vile sasa tuko kwenye dunia ya kimtandao, wosia huu nimeurekodi kwenye video na kuutupia kwenye mtandao wa YouTube, baada ya kupokea taarifa ya kifo chake. Nilipoyasikiliza tena "Mahojioano William Malecela na Pasco Mayalla" ndiyo sasa nimegundua kumbe huu ni wosia anaihusia serikali, CCM na wapinzani.

Kunapotokea msiba wowote, wafiwa wakuu wa kwanza ni familia yake, hivyo kwanza nitoe pole zangu kwa familia yake, mkewe na watoto wake. Pole kwa familia ya Mzee John Samwel Malecela, pole kwa familia yake ya JF, pole kwa wanamitandao kumpoteza mwanamtandao mwenzao. Pole kwa CCM kumpoteza mwanachama wake ambaye ni mmoja wa wana CCM Wazalendo na wakweli kabisa toka ndani ya nafsi zao. Pia pole kwa Watanzania wote kumpoteza Mtanzania mwenzetu, haijalishi alikuwa nani, thamani ya mtu ni utu, hivyo binadamu yoyote akitangulia pole ni stahiki.

Nimetokea kusoma shule ya msingi na watoto wa Mzee Malecela. Nilikuwa darasa moja na Jaji Mwendwa Malecela, huku ndugu yake Catherine (RIP) akiwa darasa moja nyuma yetu. Mdogo wake Mkwawi Ippy Malecela (RIP) akiwa madarasa mawili nyuma na dada mtu, Dk. Seche Malecela, alitutangulia madarasa mawili mbele.

Nikiwa sekondari ya Tambaza, mtoto mkubwa wa Malecela, Senyagwa (RIP), alikuwa kidato cha tano, akisoma masomo ya mchepuo wa Fizikia, Kemi ana Hisabati (PCM) na nikiwa kidato cha tatu, Dk. Seche Malecela alikuja Tambaza kusoma Kemia, Fikizia na Baiolojia (PCB).

Mwendwa tukaja kukutana naye tena kwenye fani ya sheria, maana mimi japo ni mwandishi wa habari wa kujitegemea kwa kujitolea pia ni mhitimu wa shahada ya sheria toka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na wakili wa kujitegemea.

Mmoja wa marafiki zangu akawa ana uhusiano na binti mwingine wa familia hii, Dk. Irene (RIP). Nikaja kuwa mshereheshaji (MCO wa harusi ya binti wa Malecela. Kote huko sikuwahi kufahamiana na William hadi nilipokwenda New York, Marekani kwenye Ubalozi wetu Umoja wa Mataifa (UN) , ndipo nikatambulishwa kwa shemeji yetu, mke wa Le Mutuz, ndipo nikamfahamu William.

Tukaja kukutana tena na William kwenye Mtandao maarufu kabisa wa kijamii nchini Tanzania, kuliko mitandao yote, yaani Jamii Forums au kwa kifupi JF. William Malecela alipokuja kugombea ubunge wa Bunge la Africa Mashariki (EALA), akanitafuta, nikampa sapoti. Kuna wakati nikiwa Dodoma akanikaribisha nyumbani kwa Mzee Malecela kisha tukasafiri wote kwa gari binafsi kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam. Hapo ndipo nilipomjua William kwa karibu zaidi na kwa ukweli zaidi.

Mimi na William tukawa marafiki, tukikutana viwanja tofauti tofauti vya burudani, na kama vilivyo vikombe kabatini, kuna wakati tulipishana kauli. Alikuwa mwepesi kukasirika. Mtu mkweli akikasirika, hachelewi kukiwasha ila pia mwepesi kusamehe. Kumbe William si mlevi, hanywi pombe, wala havuti sigara. Hili tunafanana, maana hata mimi situmii vilevi hivyo lakini tulipenda starehe na burudani hizi na zile. Tuliishi kwa kuponda raha kwa starehe za kula, kunywa kama vile tutaishi milele huku kila siku ukiufurahisha moyo wako kama utakufa kesho. Kwa hiyo kula raha leo, kula vizuri, lala pazuri, pata raha leo, kesho itajijua yenyewe.

Ni William Malecela, Le Mutuz, ndiye aliyenitambulisha kwenye mtandao wa YouTube na video yangu ya kwanza kwenye YouTube ni ya mahojioano na William Malecela ambayo ndio sasa wosia ambao ametuachia milele. Nataka wana CCM wote hasa viongozi, wausikilize usia huu na kuuishi.

CCM ina taratibu zake za ukosoaji kufanywa na wanachama wake. Inataka ukosoaji wowote wa CCM, ukifanywa na mwana CCM, ufanyike kwenye vikao vya ndani. William alikuwa hakopeshi.

Siku hizi kupitia mitandao ya kijamii, kumeibuka vikundi vya kusifia vikiijiita machawa. William Malecela ni mwana CCM, aliyeipenda CCM kwa dhati ya moyo wake na kiitetea kwa nguvu zake zote ila hakuwa chawa kwa sababu pia aliikosoa CCM waziwazi na si kupitia vikao vya ndani.

Ni katika mahojiano hayo, William alitoa usia mzito kwa serikali, wapinzani na kwa CCM. Je William Malecela alitoa wosia gani kwa serikali, wapinzani na kwa CCM?.

**Tukutane Jumapili ijayo**

**Paskali**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Hakika cheo ni dhamana kising'ang'aniwe tu



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

TUFANYE umefiwa na mwenza wako wa ndoa. Wewe sasa ni mjane au mgane. Umeachwa na watoto kadhaa wadogo ambao hawajawa tayari kujitegemea, hivyo kuhitaji msaada wako.

Nawe unaona ni kazi na mzigo mzito kuubeba tofauti na mwenza wako alipokuwapo, hivyo unatafuta usaidizi kwa ndugu zako, unaomba wakupe angalau vijana wawili wa kukusaidia kulea.

Ndugu zako wanakupa mvulana na msichana, unawachukua na kukaa nao, wakusaidie kulea wanao katika mazingira mazuri yenye maadili lakini wakihakikisha mahitaji na haki zinapatikana kwao.

Maisha yanakwenda kama kawaida, unaridhika kwamba sasa hutakuwa na changamoto ya kufikiria wanao wanaishije hapo nyumbani, kwani una wasaidizi uliowaamini.

Unakwenda kwenye majukumu yako ya kutafuta riziki ikiwa ni pamoja na yale yanayokulazimu kusafiri nje ya mkoa na hata ya nchi, ili mradi mikono yenu iende kinywani na wanao wauone mlango wa choo.

Lakini siku moja ghafla, unarudi nyumbani usiku, unakuta mezani kuna chakula hakijaliwa na baadhi ya wanao wamelala. Mmoja unayemkuta sebuleni anapokuona tu analia na kukwambia wengine wamelala bila kula.

Unakimbilia chumbani walimolala, kweli unawakuta wamelala fofofo tena wakikoroma lakini hawajala. Moyo unakuuma na kujiuliza ni nini kimetokea. Unawaacha kwanza ufanye uchunguzi wa kuaini kilichojiri.

Unamwuliza yule mwingine uliyemkuta sebuleni, anakwambia kuna mambo hayaendi vizuri kutokana na masharti yanayowekwa na walezi uliowachukua kwa ndugu zako.

Anasema wanataka kila unachowapa wanao nao wakipate, wasipokipata wanawapora na kuwaonya wasiseme. Si nguo si chakula na hata zawadi unazoleta, hususan unapokuwa umetoka ughaibuni.

Inakuuma, unakwenda kuwagongea mmoja baada ya mwingine, unaanzia kwa wa kike, unamhoji anakwambia wala hakuna tatizo ila wameamua kuacha tu kula kwa sababu wameshiba.

Unakwenda kwa yule wa kiume, yeye anajifanya hajui linaloendelea na unapombana zaidi, anakwambia wanasimamia watoto hao kwa zamu na leo ilikuwa ya yule wa kike. Nguvu zinakuishia na kurejea sebuleni.

Unaona kabisa mambo hayaendi, unawaamsha wote na kutaka kumaliza changamoto iliyojitokeza. Unawaambia fungukeni mseme kinachoendelea hapo ndani bila woga wala vitisho. Wanafunguka mmoja baada ya mwingine, wakielezea kuchoka kuishi na wasaidizi hao kwani ni unyanyasaji mtupu na wanakudanganya kuwa mambo yako shwari, lakini kumbe sivyo. Mmoja anasema wa kiume anawatishia kuwa kama hawataki maisha hayo, waondoke wakaishi kwa mjomba wao. Unajiuliza inafikiaje hatua mtu kuwaambia wanao wahame nyumbani wakaishi kwa mjomba! Inakuumiza na kuamua kuwasema hao watoto wa ndugu zako na kuwaonya, huku ukiwabembeleza watoto wako wale kabla ya kulala.

Wanakula lakini wakisisitiza lazima ndugu zao hao waondoke, wawaache wao wataabike hivyo hivyo bila mzazi mmoja, lakini watavumilia kwa kuwa ni mapenzi ya Mungu na kama hutaki kuwaondoa, basi wakae bila kula kama wale waumini wa Shakahola kwa Baba Paulo MacKenzie.Hili ni sawa na kilichotokea hivi kariubuni Kariakoo, Dar es Salaam, wafanyabiashara walipoamua kuweka mgomo na kufunga maduka yao kwa madai mbalimbali, yakiwamo ya utitiri wa kodi na utendaji mbovu bandarini.

Wakati wanatangaza na kutekekeza mgomo huo wakisema hautakuwa na ukomo, huku wakifunga maduka, bungeni taarifa zikadai kuwa hakuna maduka yaliyofungwa na kama yapo ni hiari ya mmiliki na si mgomo.

Taarifa hiyo ikawa imetolewa na mtu aliyepewa dhamana ya kulea wafanyabiashara hao, huku wabunge wengine akiwamo Spika, wakitilia shaka na kutaka kupata maelezo sahihi ya nini kilikuwa kinaendelea.

Kumbe Kariakoo mambo yakawa si mambo mpaka Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akaamua kufunga safari ya Dodoma-Dar kuwasikiliza wafanyabiashara ili kujua kulikoni.

Kweli akakuta maduka yamefungwa na jamaa wako nje tayari kwa lolote mpaka kieleweke. Kwa busara na hekima alizojaaliwa, Majaliwa akakubaliana nao kuonana na kuzungumza nao siku nyingine, kwanza akamzike 'Berna' Membe kijijini Chiponda.

Aliporejea akazungumza nao Mnazi Mmoja tena kwa uhuru na uwazi mkubwa, huku wakipewa fursa ya kufunguka. Kama wale watoto waliolala njaa, wakafunguka mpaka kuwakataa walezi wao wawili wa kike na wa kiume, waliokuwa hapo hapo mkutanoni.

Ina maana walezi hao walishindwa kuwalea, kumbe mmoja ndiye alisema hakuna maduka yaliyofungwa kwa mgomo na mwingine ndiye aliyekuwa akiwaambia kama hamridhiki hamieni kwa mjomba (Burundi) huku akiwafananisha na waganga wa kienyeji asiotaka kuzungumza nao

Kwa hali ya kawaida, ningekuwa mimi, walezi hawa ningewaondoa mara moja, au kwa kusemwa vile na watoto wangefugasha virago tu wakajiondokea, kwa sababu kuendelea kuwa nao kutafanya wanangu wasile tena na hivyo kulala na njaa. Hakika hawa wasipoondoka, wafanyabiashara watafunga tena maduka!

**Tujihadhari!**

# Uzinduzi wa Ikulu Chamwino Dodoma




Rais Dk, Samia Suluhu Hassan (mbele kulia), akivuta kitambaa ikiwa ni ishara ya ufunguzi rasmi wa jengo la Ikulu ya Chamwino, Dodoma jana, wengine mbele kabisa ni Makamu wa Rais Dk, Philip Mpango.



Rais Dk, Samia Suluhu Hassan, akimwagilia maji mti aliopanda katika eneo la Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma baada ya kuizindua jana



Rais Samia Suluhu Hasan akikagua gwaride maalumu lililoandaliwa na Jeshi la Polisi kwenye ufunguzi wa jengo la Ofisi ya Ikulu Jijini Dodoma jana.



Wananchi wakitoka katika uzinduzi wa Jengo la Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma jana.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan (kushoto), akimkabidhi tuzo, Janeth Magufuli, mke wa Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli kwa kutambua mchango wake ujenzi wa jengo la Ikulu Chamwino Dodoma, tuzo hiyo ilitolewa jana wakati wa ufunguzi wa jengo hilo. **PICHA ZOTE: IBRAHIM JOSEPH.**

# MAISHA

MEI 21, 2023
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
*Jumapili*

Ukurasa 14




## JUISI YA UKWAJU NA FAIDA LUKUKI

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



Rembesha uzio kupendezesha nyumba yako




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# HARUSI

Ukurasa 12


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | ■ | U | M | B | W | A |
| H | ■ | ■ | ■ | W | ■ | K |
| A | ■ | D | U | A | ■ | W |
| K | A | A | ■ | T | I | A |
| A | ■ | K | O | O | ■ | T |
| N | ■ | W | ■ | ■ | ■ | U |
| I | N | A | M | A | ■ | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


ZII, BEI, MJI, BUU, UMIMI, ZUBAA, AMANI, SAUTI, TAMBUKA, INGIZWA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

TAFUTA NJIA KUTOKA **A** KWENDA KWENYE BOKSI LA ZAWADI




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MZUNGU mmoja alionekana kumdharau Mbongo, akamwambia waulizane maswali na akishindwa anampatia Sh. 5000 na endapo yeye atashindwa atatoa 100,000.

**Mzungu:** Nchi ipi ilishindwa kwenye vita kuu ya kwanza ya Dunia?

**Mbongo:** akashindwa akatoa 5000 kuashiria hajui.

**Mbongo:** Kitu gani kikienda juu kina miguu minne na kikirudi chini kina miguu mitatu?

**Mzungu:** akafikiria akakosa jibu akatoa 100, 000, kuashiria hajui ila akataka kujua, akauliza ni nini hicho?

**Mbongo:** Akatoa 5000 kuashiria hata yeye hajui!.

**SWALI**

Samaki aina ya Pweza ana mikia mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mwanamume mchepuko asikutoe kwenye hatma ya maisha yako

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kupata vionjo vya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wakati wengine wanatamani kuingia kwenye ndoa, wako wanaoteseka mioyo inaumia. Lakini pia wako waliovumilia wakashindwa na kuchomoka kunusuru maisha yao!

Wako wanaume wanaozikimbia ndoa zao na kuanzisha uhusiano mpya, na kinamama kadhalika wanaondoka na kwenda kuanzisha maisha mengine. Na uamuzi huu wote hutokana na sababu mbalimbali zinazotolewa na wahusika.

Kuna wakati natafakari kwa nini ndoa zinafungwa kwa shamrashamra nyingi, maisha yanaanza vizuri, wanapatikana watoto, yanapatikana magari na nyumba nzuri lakini bado ndoa hizi husambaratika?

Hata hivyo, nimegundua kuwa wako maadui hushambulia sana ndoa. Adui hawa huibuka pale ndoa zinapokuwa katika utulivu, hivyo kuzusha tafrani, hofu, tamaa, kutokuaminiana na kadhalika. Kibaya zaidi, nyingi ya ndoa hizi ni changa zenye watoto wasiozidi wawili.

Hebu msomaji wangu sikia kituko hiki halafu utatoa maoni yako nini kifanyike. Dada mmoja amekaa katika ndoa yake miaka mitano sasa na amebahatika kupata watoto wawili. Mumewe ni mfanyakazi taasisi moja kubwa ya kiserikali.

Ni mtu wa kusafiri kwani hupangiwa majukumu sehemu mbalimbali nchini. Anapokuwa mikoani hujitahidi angalao mara moja kwa mwezi huja kwa mkewe kuwaona watoto. Amempa mtaji mkewe kujishughulisha na ujasiriamali asikae bure.

Matumizi yote ya nyumbani anatoa na pia humpa mkewe kiasi fulani cha fedha kila mwezi kwa ajili ya dharura yoyote anapokuwa hayupo. Ni baba anayeihudumia familia yake vizuri.

Mama huyu alishaizoea ratiba ya mumewe kuja nyumbani kila anapopata nafasi. Lakini ikapita miezi mitatu bwana hajafanya safari yoyote kuja kuiona familia yake mbali na kuwasiliana nao kwa simu.

Mama machale yakamcheza. Mbona jamaa yangu haji tena nyumbani kulikoni? Bibie akapanga kwenda kumfuata huko huko. Akakata tiketi ya basi na kumjulisha kuwa anakuja. Bwana akamwambia karibu.

Bibie kufika, kila akipepesa macho anaona jinsi mazingira yalivyo mazuri, nguo za mumewe zimepangwa vizuri. Kila kitu kipo vizuri hakuna hata chombo kichafu. Akahisi kuwa lazima yupo mtu anahudumia nyumba ile kwani anamjua mumewe ni rafu hutupa vitu ovyo!

Akawa mpole. Kingine alichogundua ni mume wake kutomchangamkia kama ilivyokuwa kawaida yake. Akimsemesha anajibu mara moja na kukaa kimya, hakuna changamko la mtu na mwenzi wake. Akajiuliza maswali lukuki bila majibu!

Hata hivyo, jawabu la maswali yake akalipata usiku wakiwa wamelala. Wakati wanandoa hawa wakiwa chumbani usiku, simu ya mume ikaita, akapokea akawa anajibu; "Sikuja kula kwani nilikuwa nimeshiba". Swali lilikuwa mbona leo hukuja kula? Na hii ilikuwa ni sauti ya mwanamke ikiuliza kwa upole!

Jamaa akamsihi mwanamke huyo, "tuongee kesho muda huu nalala". Akakata simu. Baada ya hapo hali ya hewa ilibadilika na usiku ule ulikuwa mchungu sana kwa bibie. Ndipo alipobaini kuwa ule usafi aliouona mle ndani kumbe yupo anayependezesha!

Japokuwa mama huyu alikaa na mumewe siku mbili na ile ya tatu akaondoka, lakini bado moyo ulikuwa unaumia kwani alishajua kuwa muwewe ameshatekwa ufahamu ndiyo maana hamchangamkii kama awali.

Ama kweli Maisha Ndivyo Yalivyo Andiko moja la Mungu linasema, ajidhaniaye amesimama na aangalie asianguke. Msemo mwingine unasema ukiona mwenzio anayolewa, wewe tia maji, ujiandae.

Watu wengi huyaona matatizo yanayowakumba wenzao, baadhi wakichekelea na kushangilia kana kwamba wao jambo hilo haliwezi kuwapata. Upo mzunguko wa matatizo ambao huwapata watu wengi na kuonekana kukaribia kufanana.

Ndiyo. Linipatalo mimi laweza pia kukupata wewe, labda tofauti ni jinsi ya kulitatua ili kupatia ufumbuzi. Ndoa inavunjika kumbe ni roho ya wivu, roho ya mitala (kuoa wake wengi), hasira, mizimu ya mababu, roho ya majini mahaba na kadhalika.

Mama huyu niliyemzungumzia hapa, alijiamini kuwa mume wake hawezi kuwa na mahusiano nje ya ndoa kwa jinsi alivyokuwa anamtunza. Kumbe sivyo. Alivyomfuata tu, akakutana na majibu yake.

Unadhani mwanamke huyu atakuwa katika hali gani? Ule uaminifu alioujenga kwa mumewe tayari ulitiwa dosari. Majaribu yanapofikia hapo, ndipo mwanamke anapaswa kujitia nguvu kwa BWANA, Mungu wake.

***Wiki ijayo nitaeleza zaidi kwanini anapaswa kujitia nguvu. Je, una kisa? Ujumbe 0715268581*** .

## WARAKA WA NDANI



Na Godfrey Mushi

# Bila TTB, TFS hawawezi kuutangaza Msitu wa Rau kimataifa

MAWAZO huishi hata ukiwa kaburini hasa kwa mtu unayefikiri zaidi kuacha alama duniani. Nimeanza na kumbukumbu hiyo kwa sababu nimemkumbuka mtafiti na mwanasayansi wa wanyamapori, marehemu Dk. Jane Goodall, aliyeanzisha wazo la kuwa na Roots & Shoots, kwa ajili ya kuifanya dunia kurejea edeni na kuwa mahali pazuri pa kuishi kwa viumbe wote.

Wakati wa uhai wake akiwa Tanzania, alipigania sana ustawi na uhifadhi wa mazingira, wanyamapori na viumbe wengine walioko kwenye hatari ya kutoweka katika mapori tengefu, mapori ya akiba na hifadhi za taifa.

Aliijua Tanzania, alijua umuhimu wa rasilimali hii muhimu na adhimu. Kama ndivyo, kwa nini hatumuenzi kwa kuhuisha matamanio yake katika mazingira na uhifadhi wa Msitu wa Rau; ambao haujatangazwa na watalii wanaoingia nchini wakaamua kwenda kuutembelea na kujifunza mengi?

Nani anajua kwamba Hifadhi ya Msitu wa Rau, maarufu msitu wa Njoro, ulioko chini ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwamba ndio msitu wa kwanza kuwa ndani ya mji nchini Tanzania?

Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), bebeni jukumu lenu la kisheria la kuitangaza Hifadhi ya Msitu wa Rau. Kuna mahali kama taifa tunajisahau kutangaza vivutio vyetu na tunachukulia eti ni vidogo vidogo, kumbe vikitumiwa vizuri vinaweza kuongeza mapato ya sekta ya utalii nchini.

Urithi huu tunapaswa kuviriithisha vizazi vijavyo, licha ya kwamba msitu uko katikati ya Mji wa Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro. Una maajabu mengi na haujatangazwa kama vivutio vingine vilivyoko kaskazini mwa Tanzania.

Ni eneo la maajabu, lina kitu kinachoitwa Ndiwa ya Uru, yaani Bwawa la Mizimu. Kihistoria hapo ndiko wananchi wengi hasa kabila la Wachaga, hupendelea kwenda kufanya matambiko yao.

Wenyeji wa Kilimanjaro, kuanzia Uru, Old Moshi, Kibosho, Machame na Siha na sehemu nyingine za Kilimanjaro, huenda hapo kufanya matambiko ili kuondoa mikosi, kupata mali au utajiri na kupona magonjwa.

Wako wanyamapori wa aina mbalimbali, isipokuwa wale wanyama wakubwa watano, lakini katika hifadhii hii kivutio kikubwa ni chatu mkubwa ambaye mara nyingi huwa anatokeza nje ya hifadhi kuelekea yalipo makazi ya wananchi ila hana madhara.

Chatu huyo huwa anatokea zaidi upande wa Kijiji cha Msasani na Kaloleni. Huyo chatu ni mkubwa zaidi kiumbo na inaelezwa ana utamaduni wa kuonekana kila ikifika saa 5:00 asubuhi na si muda mwingine. Huwa anatoka msituni kwenda nje ya hifadhi eneo la uraiani anaota jua na watu wakitokea wakimwona wakipiga kelele, anarudi msituni na hadhuru wanaopiga kelele.

Vijiji vitano vinavyouzunguka msitu huo vinalindwa na historia ni Msasani, Mji Mpya, Mandaka, Mabogini na Msaranga. Msitu huo unaundwa na Kata za Mabogini, Msaranga na Mji Mpya.


Achilia mbali vivutio hivyo, Hifadhi hiyo hiyo ya Rau, ina mti mkubwa ambao ni mti wa mvule. Ni mkubwa na wa kwanza kwa unene katika nchini zote saba za Afrika Mashariki. Huo mti haukuoteshwa ila ni mti wa asili, na una zaidi ya miaka 200.

Ukubwa wake ni kipenyo 300 na kama ukitaka kuushika ni lazima muuzunguke kwa kuushikana mikono watu 13. Lakini hapo hapo pia, kuna miti ambayo haipatikani Afrika Mashariki yote, inaitwa Ostig Mamsoo. Zamani hiyo miti ilikuwepo nchini Kenya, na iliteteketezwa na majangili na sasa imebaki pekee katika Msitu wa Rau.

Inaelezwa kwamba Msitu wa Rau kwa sasa una hekta meta 584, zamani ulikuwa na hekta meta 2,000 lakini kutokana na makazi ya jamii kuongezeka ilifikia mahali walipokuwa wengi kukajitokeza ugomvi ukamegwamegwa na kubakia kiasi hicho.

Mbali na mambo hayo, una utajiri wa chemichemi nyingi ambazo zinafua maji yanayotoka ndani ya hifadhi kwenda kulisha mashamba zaidi ya hekta 8,800 za mashamba ya umwagiliaji yanayouzunguka.

***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***









Jukumu la kuandaa sherehe ya harusi ni wanandoa
Maharusi mnatakiwa kuandaa mpango wa sherehe mapema kabla ya ndugu na watu wengine kuwaandalia.
Kuna watu watashtuka kuhusu hili ila sherehe ni ya kwenu ninyi maharusi na sio ya ndugu mliowaalika kwenye kamati.
Maharusi wengi hawafahamu jukumu hili, wanafika kwenye vikao hata bajeti ya sherehe tu hawana, wala hawajui wanataka kupata wageni wangapi na iweje.
Matokeo yake sherehe nyingi za harusi huandaliwa na mawazo ya kamati bila kujali itafana au laah.
Jukumu la kamati ni kufuatilia michango na kupeana kazi za kufanya wakati wa sherehe tu.

# MITINDO

Na Mary Geofrey



## Ongezea umaridadi kwa kuvaa Skafu

UVAAJI skafu wengi tunaujua wa kuvaa shingoni mara nyingi ila unaweza kuvaa skafu kwa mitindo mingine mingi.

Unaweza ukafunga kama kilemba au kama urembo kwenye 'handbag' yako pia.

Unaweza pia ukavaa kama belt tumboni, njia zote hizi ili mradi tu kupendeza kuongezea mvuto kwenye kivazi chako.

Skafu yako unaweza kuivaa shingoni nyakati zote za baridi au kiangazi kwa sababu zipo nyepesi na nzito pia.

Skafu ukiivaa shingoni inaongeza umaridadi na inakamilisha muonekano wako. Kuna namna nyingi za kuvaa skafu na kuonekana maridadi zaidi kuliko usingevaa.

Lakini pia skafu zinavaliwa na watu wa rika zote wanawake kwa wanaume kama ambavyo picha za mionekano tofauti ya watu waliovaa skafu na kuonekana nadhifu zaidi.







URAMBO

## UREMBO

Na Mary Geofrey

# Njia rahisi ya kumaliza chunusi



WATU wengi wamejikuta wakitumia vipodozi vyenye kemikali siyo kwa sababu ya kupenda isipokuwa kukosa ushauri sahihi.

Leo tutaelekezana namna ya kumaliza tatizo hili kwa kutumia njia za asili kabisa bila kutumia vipodozi vyenye kemikali.

Magadi Soda

Magadi soda ni mazuri kwa kusafishia uso na hasa ukiwa na chunusi. Changanya kiasi kidogo cha magadi soda na maji ya kutosha kuunda kidonge kidogo na kisha weka au kandika kidonge hicho sehemu ilioathirika na chunusi.

Kwa muda wa dakika 15-20 au mpaka ikauke na kisha suuza kwa maji ya baridi.

Unaweza kurudia rudia mara kadhaa kwa siku mpaka utakapo ona athari ya chunusi imepotea.

Matango

Unaweza kutumia Tango kwa kuondoa chunusi na hata kuondoa mabaka mabaka katika ngozi na kuifanya ngozi yako kuonekana yenye afya na yenye kuvutia.



Matango ni mazuri sana kwa kusafishia uso na hasa ukiwa na chunusi. Kata tango na kisha lipondeponde (unaweza kutumia blenda) kisha paka au kandika usoni. Acha ikae kwa muda wa dakika 15-20 kisha suuza kwa maji baridi. Unaweza kurudia kwa siku mara mbili mpaka mara tatu kwa siku.

Kitunguu swaumu

Unaweza kutumia kitunguu swaumu kuondoa chunusi, matumizi ya kitunguu swaumu, huleta matokeo mazuri sana kwa kuondoa chunusi usoni na hata kuuwa bacteria kwasababu kina kemikali (antiseptiki) inayozuia kukua kwa bakteria kwenye jeraha au ngozi iliyo athirika kwa chunusi au hata kwenye kidonda. Na pia ina viwango vya juu wa salfa (ni zuri kwa ajili kukausha mafuta kwenye ngozi ya mwili). Twanga kitungu thaumu, au unaweza kukata nusu na kubandika sehemu iliyo na chunusi shikilia kwa dakika 5-10, na kisha safisha na maji baridi rudia asubuhi na jioni.



## MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya ukwaju na faida lukuki

**Mahitaji:**

-Maji ya moto lita moja, ukwaju wa kutosha na jagi au birika lenye uwezo wa kutosha maji lita moja au zaidi.

**Jinsi ya kutengeneza**

Weka maji yako ya moto kwenye jagi au birika kisha weka ukwaju ndani yake (ukwaju uliotolewa maganda).

Acha ukwaju ndani ya maji ya moto kwa muda hadi maji yatakapopoa kabisa.

Baada ya hapo koroga mchanganyiko huo hadi uhakikishe kuwa juisi imekuwa nzito.

Kisha mimina juisi yako kwenye jagi lingine kuchuja mabaki ya ukwaju (usichuje juisi kwa chujio la chai).

Baada ya hapo juisi yako itakuwa tayari kutumika. Lakini usiweke sukari wala kitu kingine chochote kwenye juisi hiyo.

Sasa unaweza kuanza kunywa juisi yako. Sio lazima uimalize yote kwa mkupuo, lakini hakikisha kuwa unaimaliza ndani ya dakika kama 10 hadi 15.

**Matokeo**

Baada ya kuimaliza juisi hiyo na kukaa kwa muda wa kama nusu saa au zaidi utaanza kuona mabadiliko kwenye tumbo lako.

Tumbo litavurugika na utaanza kuharisha mara kwa mara na hapo ndio dawa inafanya kazi ya kusafisha tumbo.

Jitahidi kama utaweza jiwekee utaratibu wa kunywa juisi ya aina hii angalau mara moja kila mwezi kwani haina gharama na haina madhara mwilini.





MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

## Zingatia haya kuboresha maliwato

Na Restuta James

KAMA nilivyoeleza wiki iliyopita, bafu au choo ni sehemu ngumu kidogo kuipamba kutokana na kuwa na vitu vingi visivyohamishika.

Wataalamu wa mapambo ya ndani, wanaeleza kuwa zipo njia nyepesi na rahisi za kulifanya bafu lako lionekane maridadi wakati wote, wakishauri kuzingatia uasili katika kazi hiyo.

Aidha, njia zipo nyingi kufanikisha hilo lakini wanapendekeza njia zinakazoifanya maliwato kuonekana safi na yenye mpangilio maridhawa wakati wote.

Hakikisha henga ya kuweka 'toilet paper' inamudu kubeba walau rola mbili. Wataalamu wanaeleza kuwa kuziweka mbili kunaongeza mwonekano mzuri zaidi.

Wanashauri kwamba sehemu hiyo iwe pia na 'kidroo' cha kuweka jarida maridhawa. Hii itamfanya mtu anayengia chooni asiwe 'bored' au asibaini mapungufu yaliyopo.

Wataalamu hao wanapendekeza pia kwamba juu ya kidroo hicho unaweza kuweka mshumaa wako wenye harufu nzuri au manukato mahsusi kwa chumba hiki.

"Muhimu zaidi ni kuhakikisha kwamba mapambo haya yanakwenda sambamba na ua lililopandwa japokuwa unaweza kuweka ua la kutengeneza," anasema mtaalamu wa mapambo ya ndani.

Kuhusu ua, wataalamu wanashauri kuweka yale yanayoweza kusafisha hewa na kuleta utulivu kwenye akili uwapo eneo hilo.

Wanashauri kwamba bafuni au chooni ni sehemu ya kuweka vitu 'vidogovidogo' ambavyo ni nadra kuvikuta kwenye maeneo mengine.





# Rembesha uzio kupendezesha nyumba yako

UZIO ni moja ya sura ambazo hutumika kama urembo wa nyumba kulingana na namna mhusika anavyotaka uwe kwa kutegemea na bajeti au ubunifu unaotumika kuutengeneza.

Kwa ujumla, nyumba inapozungushiwa uzio iwe ni kwa ajili ya ulinzi, usalama, faragha au mwonekano, unasaidia pia kuongeza thamani ya nyumba husika.

Kwa mazingira yetu ya kitanzania, kuna uziio wa aina mbalimbali ukiwamo za matofali, mbao, miti, makuti, chuma, aluminum, wavu na mabati.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Stephen Kennedy, anasema kuna mambo ya kuzingatia kabla ya kuweka uzio wa nyumba yako.

Anasema ni vyema ukaepuka kukurupuka kuchagua uzio kabla hujafahamu gharama za utunzaji wake na kwamba endapo utaamua kimakosa, kuna uwezekano wa kuharibu mwonekano wa sura ya nyumba yako hata kama ni nzuri kiasi gani.

"Kwa mfano unapoweka uzio wa mbao, unatakiwa ujue kwamba unatakiwa kupakwa rangi mara kwa mara na ujue zinaoza pia baadaye. Kwa hiyo zinahitaji maboresho ya kila mara kwa sababu pasipo kufanya hivyo zinaharibika, hivi ni vitu ambavyo unapswa kujua katika kila aina ya uzio unaotaka kuweka," anasema Kennedy.

> **"Anasema ni vyema ukaepuka kukurupuka kuchagua uzio kabla hujafahamu gharama za utunzaji wake na kwamba endapo utaamua kimakosa, kuna uwezekano wa kuharibu mwonekano wa sura ya nyumba yako hata kama ni nzuri kiasi gani.**


Jambo linguine, anasema kabla ya kutengeneza uzio wako unatakiwa ufahamu unatakiwa uwe kwa mtindo gani.

Anashauri kwamba uzio wa kurembesha zaidi katika lango kuu ikiwamo kuweka taa za rangi husaidia kuweka mwonekano mzuri wa ukuta na nyumba kwa ujumla.

Kennedy anashauri kuweka uzio wenye kuleta faragha na wa kuimarisha ulinzi katika nyumba na si bora uzio.

Anasema uzio unaoacha nafasi au matundu katika nyumba hauna faragha na wala hauwezi kukulinda vya kutosha, ila unakupa starehe ya kuangalia kinachoendelea nje ya makazi yako unapokuwa umejipumzisha.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
'UDAMBWIDAMBWI'
JUKWAANI
NAACHA USHABIKI RASMI
NAYAPORO-MOSHA NJIA YOTE KUANZIA DAR' HADI MWANZA BILA KUPOA!
NASHUKURU WAZEE NIMEFIKA SALAMA DA'SLAMU NIMEANZA 'KUBANGAIZA' ILA KUNA WAGAMBO WENGI HATUKAI CHINI!
'WAGAMBO WASAFI SANA WAMEWAPA HADI VITI?' MJINI KUZURI
TUSHATOSHANA NGUVU ULINGONI SASA MBONA BADO UNANIFATA HUKU NAKOKWENDA?
'UMESAHAU KAMA ULITEMBEA NA MKE WANGU? TUMEMALIZA ULINGONI LAKINI ROHONI MIMI BADO SIJAMALIZA LAZIMA LEO LIFE JITU!
ENZI ZANGU HAKUNA STAREHE NISIYOIFANYA NDIO MAANA HADI LEO SINA NYUMBA WALA KIBANDA NIMEPANGA NA NADAIWA KODI. 'MILIONI SAMANINI NIMEICHAKAZA"
NA BADO HUJADAIWA KODI 'I WISH' NINGE-PAJUA ULIPOPANGA!
MIJITU KAMA HIYO NDIO ILIKUWA INA-KUPIGA INAKULIPA!
ALAFU UNANUKA DOMO
SASA YANINI UDAIWE KODI SI UENDE UKALALE HUKO ULIPOKUWA UNAZICHAKAZA HELA ZAKO? BWEGE WE
ALAFU JAMANI HELA YA KIINUA MGONGO INA MASHETANI MSIBISHE INAISHIAGA HUKO!
MSITUTIE WEHU SISI WAPOKEA VIINUA MGONGO WATARAJIWA TUZIKATAE HELA ZETU
TOA NAULI KABISA
FANYAKAZI ZAKO LAKINI LEO UKIRUDI NATAKA UJE NA JIBU "EMI. EVA, JUDI, JOI NA FETI MPAPA NI NANI WAKO"
MTUMEEEEEEH! LEO NIMESAHAU KWENDA NA SIMU BAFUNI...SITOBOI KAMA SIJAENDA KIBASILA ITAKUWA SEWAHAJI...
NAKIRI MKE WANGU SAFARI HII MGANGA HUJAPATA, NATOKA NA SHOGA'AKO HUNIFUMANII?
NIMEACHA KUTUMIA WAGANGA ILA MUMEWE ANAKUTAFUTA NA RAFIKI ZAKE WAMENUNUA MAFUTA WANAKUTAIMU.
...KINYUNYIZO CHA LEO...
UKICHEZEA MVUA USIOGOPE KUTETEMEKA BARIDI...

## HABARI KIMATAIFA



Viongozi wa nchi za G7 wakiwa katika picha ya pamoja katika Mnara wa Kumbukumbu ya Amani wa Hiroshima, **PICHA: MTANDAO.**

# Marekani kuruhusu washirika kuisaidia Ukraine ndege vita

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imesema itawaruhusu washirika wake kuipatia Ukraine ndege za kivita za hali ya juu, zikiwamo za F-16 zilizotengenezwa Marekani, katika kuimarisha zaidi usalama dhidi ya mashambulizi kutoka Russia.

Mshauri wa Usalama wa Taifa wa Marekani, Jake Sullivan, alisema jana kuwa Rais Joe Biden aliwajulisha viongozi wa kundi la G7 juu ya uamuzi huo juzi katika mkutano wa wakuu wa nchi hizo unaofanyika Japan.

Alisema wanajeshi wa Marekani pia watawapa mafunzo marubani wa Ukraine kutumia ndege hizo.

Ukraine kwa muda mrefu imekuwa ikitafuta ndege za teknolojia ya juu na Rais Volodymyr Zelensky alipongeza hatua hiyo kama uamuzi wa kihistoria.

Marekani inapaswa kuidhinisha kisheria uuzaji upya wa vifaa vilivyonunuliwa na washirika na hatua hiyo itasafisha njia kwa mataifa mengine kutuma hifadhi zao zilizopo za F-16 kwa Ukraine.

"Katika kipindi cha miezi michache iliyopita, sisi na washirika wetu tumezingatia sana kuipa Ukraine silaha zenye kutumia mifumo na mafunzo inayohitaji kufanya operesheni za kushambulia msimu huu,"

Sullivan aliwaambia waandishi wa habari katika jiji la Hiroshima na kuongeza kuwa: "Tumetimiza kile tulichoahidi." "Sasa tumegeukia mijadala kuhusu kuboresha jeshi la anga la Ukraine kama sehemu ya dhamira yetu ya muda mrefu ya kujilinda kwa Ukraine. Mafunzo yanapoendelea katika miezi ijayo, tutashirikiana na washirika wetu kubainisha ni lini ndege zitawasilishwa, nani ataziwasilisha na zitakuwa ngapi," aliongeza.

Ukraine imerudia mara kadhaa kushawishi washirika wake wa Magharibi kutoa ndege za kusaidia katika mapambano yake dhidi ya Russia.

Kabla ya tangazo rasmi la jana, Rais Zelensky alisema ndege hizo zitaboresha sana jeshi la anga na kuongeza kuwa anatarajia kujadili utekelezaji wa vitendo wa mpango huo kwenye mkutano wa G7 huko Hiroshima, atakapowasili leo.

Marekani ilikuwa na shaka kuhusu kuipatia Ukraine ndege za kisasa za kivita - angalau katika muda mfupi ujao.

Mtazamo wake badala yake umekuwa katika kutoa msaada wa kijeshi kwenye ardhi.

- BBC

# Waziri ataja sababu usitishaji uchimbaji makaburi Shakahola

**NAIROBI,** KENYA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani wa Kenya, Kithure Kindiki, ameeleza sababu za kusimamisha utafutaji wa makaburi kutafuta miili ya watu katika msitu wa Shakahola.

Kindiki alisema jana kuwa kazi ya kutafuta makaburi na kufukua waathirika wa mauaji ya Shakahola imesitishwa.

"Tulisitisha zoezi hilo ili kuruhusu upangaji wa vifaa vya uchunguzi wa maiti 123 za ziada zilizopatikana katika awamu ya pili ya uchimbaji," alisema.

Pia alisema awamu ya pili ya uchunguzi wa maiti itaanza Jumatano ijayo. Uchunguzi wa maiti utafanywa katika Hospitali ya Kaunti Ndogo ya Malindi.

Hata hivyo, alisema shughuli ya kuwatafuta na kuwaokoa manusura ndani ya Msitu wa Shakahola na shamba la Chakama, itaendelea bila kukatizwa.

"Pia itapanuliwa katika kingo za Hifadhi ya Kitaifa ya Tsavo Mashariki katika siku zijazo kwa kutumia utafutaji wa ardhini na ndege zisizo na rubani," alisemaght: Getty

Alisema upekuzi na uchimbaji wa makaburi hayo utaendelea tena baada ya kukamilika kwa awamu ya pili ya uchunguzi wa maiti.

-BBC

# Washuhudia moshi wa volkano Goma

**KINSHASA,** DRC

WAKAZI wa Goma katika mji mkuu wa Kivu Kaskazini, juzi walishuhudia moshi mwekundu ukifunika kreta ya volkano ya Nyamuragira, takriban kilomita 25 kaskazini kutoka katika mji huo.

Kwa mujibu wa kituo cha uchunguzi wa volkano cha Goma, mlipuko wa huo ulikuwa umetabiriwa awali kuwa ungetokea.

Kituo hicho kilisema tangu Mei 9, mwaka huu, mtiririko wa lava ulionekana ndani ya kreta ya kati na kuonyesha kwamba mlipuko ungesukuma lava kuelekea Hifadhi ya Kitaifa ya Virunga, mbali na jiji la Goma lenye wakazi milioni mbili.

Miaka miwili iliyopita, nusu ya wakazi wa jiji hilo walilazimika kuacha makazi yao wakati volkano nyingine iliyo hai ilipotokea karibu na Nyiragongo Mei, 2021 na kuua takribani watu 32.

- BBC

# Wanane familia moja wateketea kwa moto

**KAMPALA, UGANDA**

WATU wanane wa familia moja wamefariki dunia katika ajali ya moto iliyotokea katika wilaya ya Kyankwanzi, katikati ya Uganda huku wengine watano wakijeruhiwa.

Kutokana na tukio hilo, polisi katika wilaya hiyo wanachunguza ili kubaini chanzo cha moto huo.

Tukio hilo lilitokea juzi alfajiri katika Kijiji cha Kalagi B, Halmashauri ya Mji ya Kalagi- Masode, wilayani Kyankwanzi.

Polisi wamewataja waliopoteza maisha katika tukio hilo kuwa ni Juliana Mukansiime mwenye umri wa miaka 60 ambaye alifariki dunia pamoja na binti zake Mariam Nawanyana (36) na Zaituni Mukakigyeri (32).

Sambamba na mama na binti zake hao, wengine waliofariki dunia ni wajukuu zake Patricia Namubiru (8), Leticia Nsinga (6), Patrick Kisakye (2), Martine Byakatonda na Gerald Bbale, wote wana umri wa miaka saba kila mmoja.

Watu waliojeruhiwa katika tukio hilo, kwa mujibu wa polisi ni Nyabutono Mukambabuka (30), Ruth Namata (16) na mtoto mdogo wa kike aliyejulikana kwa jina la Mumbejja.

Kwa mujibu wa mwenyekiti wa Kijiji cha Kalagi B, Patrick Kyalimpa, Mukakigyeri na Byakatonda walifariki dunia muda mfupi baada ya kufikishwa katika Hospitali ya Kiboga.

Kiongozi huyo alisema wanahisi kwamba moto huo ulisababishwa na Nawanyana kwa sababu alikuwa amewekwa mahabusu kutokana na mgogoro wa ardhi wam uda mrefu baina yake na ndugu zake.

Wanafamilia hao wamekuwa katika mgogoro wa ardhi katika eneo lenye ekari sita lililoko katika Kijiji cha Kiseresi.

MONITOR

SAFU

MAKALA

# WALIPAKODI NI WATEJA SI MAADUI



Na Magabilo Masambu

**Kikulacho ki nguoni mwako, wazuri, wabaya ni hao hao**
**Na Adam Fungamwango**
**WALE waliosema hakuna kitu duniani ambacho kinafanyika hakijafanyika huko nyuma walikuwa sahihi. Ukisoma na kusikiliza hata misemo, methali za watu wa kale, maarufu kama wahenga, utagundua hilo.**

BASI utuambie, waonaje? Ni halali kumpa Kaisari kodi ama sivyo? Lakini Yesu akaufahamu uovu wao, akasema mbona mnanijaribu enyi wanafiki? Nionyesheni fedha ya kodi. Nao wakamletea dinari, akawaambia ni ya nani sanamu hii na anwani hii? Wakamwambia ni ya Kaisari. Akawaambia basi mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari na Mungu yaliyo ya Mungu. Waliposikia walistaajabu wakamwacha wakaenda zao." (Mathayo 22:17-22)

Ukweli ni kwamba masuala ya kodi hayakuanza leo bali miongo mingi iliyopita. Maandiko yanaonyesha kwamba anayestahili kulipwa kodi basi alipwe na anayestahili sadaka pia apewe sadaka yake. Maana yake kodi ya haki ndiyo inayotakiwa kulipwa, si kubambika kodi isiyostahili ili mtu ashindwe kulipa na kuanzisha mazungumzo ya rushwa.

Sheria inampa uhalali mkusanya kodi wa Tanzania kufanya hivyo lakini mazingira, hekima na busara vinatoa nafasi ya namna bora ya kuitumia sheria hiyo ili kupata fedha za kodi bila kutumia nguvu. Bahati mbaya wakusanya kodi wetu, wamekuwa wakidhani kwamba njia za nguvu zinazotumika katika kuidai ni sahihi.

Ni muhimu serikali itambue kwamba walipakodi ni wateja wao na si maadui kama ambavyo tumekuwa tukishuhudia kodi zinadaiwa kwa kutumia vikosi vya polisi. Hawa watu wanahangaika peke yao kutafuta mitaji, kwa nini kwenye kukusanya kodi iwe kama mmechangia mtaji pamoja na kwamba sheria inalazimisha kulipa kodi? Sheria hailazimishi kufanya biashara, hivyo mtu akiona ni kero anaweza kubadili kazi asifanye biashara. Kudai kodi ni lazima itumike akili yenye kutia hamasa ili watu walipe kodi huku wakiwa na furaha.

Serikali inatakiwa kuwa mlezi isiwe na jukumu moja tu la kudai, maafisa wa kodi wasiwe kazi yao kukaa tu ofisini na kwamba siku wakijisikia kudai kodi wanatoka kwenda mtaani. Kinachotakiwa wakati mwingine wanaweza kuvaa kawaida kama raia wengine bila zile tai zao ambazo watu wameshakariri kwamba ukiwaona basi ujue ni kodi. Wakishavaa kawaida wanazunguka kwenye biashara za watu kujionea wanavyofanya biashara kupiga nao stori, kisha kujitambulisha kwao na kwamba tumekuja angalau kubadilishana nanyi mawazo tuone mnakwama wapi.

Yafuatayo yakifanyika yatasaidia sana watu kulipa kodi. Moja, kila meneja wa TRA mkoa anatakiwa kuwa na orodha ya wafanyabiashara wakubwa ndani ya mkoa. Ukishakuwa na orodha hiyo basi mara kwa mara unakutana nao kujadili changamoto wanazokumbana na nazo katika ufanyaji wa biashara zao. Vikao hivyo vitawasaidia wafanyabiashara hao kueleza wapi wanahitaji msaada wa serikali ili kufanya biashara zaidi na kuwezesha kupata fedha na kulipa kodi zaidi.

Simaanishi wafanyabiashara wa kati au wadogo hawana maana lakini naamini changamoto za kibiashara za hawa wakubwa zikishatatuliwa basi hawa wa chini pia watakuwa na uwezo wa kufanya biashara vizuri na kwa wingi.

TRA kupitia vikao wasijikite kuwa wanatoa elimu ya mlipakodi pekee bali waende mbali zaidi na kutoa elimu ya namna bora ya kufanya biashara maana wafanyabiashara wengi hawana elimu ya biashara japo wanafanya biashara. Ikiwezekana pia wawaunganishe na masoko ili bidhaa zipatikane na kuuzika kwa urahisi. Vikao hivyo viwe vya mara kwa mara ili kujenga uhusiano mzuri baina ya TRA na wafanyabiashara hao.

Pili, ni muhimu kuanzisha mashindano ya walipakodi wazuri na waaminifu ndani ya mkoa. Hili litamfanya kila mtu apambane ili kuwa mlipakodi bora ndani ya mkoa.

Mashindano hayo yaambatane na zawadi kwa washindi na kwa kufanya hivyo watu wengi watajikuta wanalipa kodi vizuri. Siku ya kukabidhiwa zawadi iambatane na hafla ikiwezekana na chakula cha pamoja, kujenga uhusianao zaidi na maofisa wa kodi.

Washindi watangazwe na kutambuliwa kwa vyeti safi pamoja na zawadi zao, maana yake hata viongozi wa wafanyabiashara watatokana na washindi hawa. Ushindi huo uwe katika daraja la kwanza, pili na tatu ili hawa wa chini wawe wanapambana kuwazidi wa juu.

Tatu, ni matumizi ya kodi zetu. Ukishaanzisha mambo mbalimbali ambayo yatawafanya wafanyabiashara walipe vizuri kodi, kinachofuata ni matumizi mazuri ya kodi zao, yaonekane kwenye huduma za jamii kama afya, elimu, miundombinu lakini kubwa zaidi kutoona na kusikia kwamba kodi za Watanzania zinatafunwa na baadhi ya viongozi ambao si waaminifu serikalini.

Hata ikisikika hivyo, basi lazima hatua kali za waziwazi zichukuliwe ili kujenga imani kwa walipakodi kwamba kodi zao zinatumika ipasavyo.

Mataifa mengine wanalipa vizuri kwa sababu wanaimani kodi zinafika na zinafanya kazi zao za kijamii. Sisemi kwamba huko hakuna wakwepa kodi lakini wengi wana imani kubwa juu ya matumizi ya fedha zao. Hapa si mara moja unasikia mlipakodi anasema "kodi zenyewe wanakula tu" kwa hiyo serikali lazima irudishe imani hiyo kwa walipakodi kwa vitendo na si maneno matupu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kikulacho ki nguoni mwako, wazuri, wabaya ni hao hao



Na Adam Fungamwango

WALE waliosema hakuna kitu duniani ambacho kinafanyika hakijafanyika huko nyuma walikuwa sahihi. Ukisoma na kusikiliza hata misemo, methali za watu wa kale, maarufu kama wahenga, utagundua hilo.

Walikuwa na misemo na methali ambazo zilikuwa na maana nyingi za kufundisha, kutahadharisha, kuonya na kumuwekea yeyote kumbukumbu ya kile kinachosemwa.

Leo tutajikita kwenye kufahamu binadamu mwema na yupi mbaya. Baadhi ya watu wanaweza kutofautisha kati ya mtu mwema na mbaya.

Hata hivyo wazee wa zamani kwa sababu waliishi kabla yetu na kuyaona mengi, wao wanakwambia hakuna mtu mwema na mwingine mbaya. Yeyote yule anaweza kuwa mwema, na akabadilika baadaye na kuwa mbaya kwako. Hata mbaya anaweza kubadilika baadaye akawa mwema pia.

Yaani kwenye dunia hii hakuna rafiki wa kudumu au adui wa kudumu. Ndiyo maana wakaja na misemo na methali nyingi zinazothibitisha kile wanachokisema.

Kwanza kabisa ipo inayosema 'kikulacho ki nguoni mwako.' Maana yake ni kwamba kinachokutafuna siku zote huwa kwenye nguo yako.

Walikuwa sahihi kabisa. Ukiumwa na kunguni, papasi au chawa ujue yupo kwenye nguo yako. Haiwezekani ukaumwa na mdudu aliyeko kwenye nguo ya mtu mwingine.

Maana methali hii ni kwamba yeyote anayekuumiza, kukufanyia ubaya, au kukusaliti ni yule anayekufahamu. Anayejua udhaifu wako, unapoishi, unavyoishi, unapokwenda, unapopita na huwa mnawasialiana naye na kupeana taarifa kama rafiki mwema, ndiyo anayeweza 'kukuuza'. Akatoa siri kwa maadui zako wakakumaliza kwa njia yoyote ile. Yeyote ambaye hakufahamu ni ngumu sana kukudhuru.

Wahenga hawakupoa, wakaja na msemo wa kusapoti methali hiyo, 'wema hao na wabaya ni hao hao.'

Wana maana kuwa mtu mwema au mbaya wote hawana alama. Huwezi kujua huyu mwema na huyu mbaya. Mwema anaweza kuwa mbaya kwako, anakufanyia vitu vya ajabu kiasi kwamba hata wewe mwenyewe baadaye ukija kuambiwa ni fulani aliyekufanyia hivyo, unashtuka.

Hawa watu wa zamani wameshayaona haya tangu huko nyuma. Hii inatokea hadi kwenye kizazi cha sasa, lakini kama nilivyosema awali kuwa vitu vyote hivi vilishatokea karne na karne nyuma. Yanayotokea sasa ni marudio tu.

Hapa tunachofundishwa ni kile ambacho watu wa itelejensia wanachokiamini kuwa 'usimuamini mtu yeyote, na usiamini kitu chochote hata kama ni maiti.'

Wanamuziki wa zamani nao hawakuwa mbali. Waliyaona haya na wakatunga nyimbo mbalimbali zinazozungumzia kuhusu watu waliowaamini sana wengine kupita kiasi, matokeo yao wakayaona.

Bendi ya Juwata Jazz 'Msondo Ngoma', ilitunga kibao kilichoitwa 'Kikulacho.' Hebu tuangalie mashairi ya wimbo huu uliofyatuliwa kwenye miaka ya mwanzoni mwa 1980.

"Ulimpenda sana, ukamthamini yule kijana, ulijua ni ndugu yako, wa kufa na kuzikana, kumbe ulidanganyika, unajuta, unajuta sasa. Kumpenda mtu adui, ona sasa unateseka. Kaa ujue, adui hayupo mbali nawe, hujigeuza leo mtu na kesho chui, huyo adui. Leo unakula naye na kesho unacheka naye, usimuamini sana, mtu yoyote.

Nilikueleza, tangu mapema, ndugu yangu hukuniamini, leo mwenyewe umeyaona, kikulacho ki nguoni mwako waswahili walisema.

Ndugu yangu ni kweli yale uliyonieleza, nilidhani unanigombanisha na yule kijana.

Makucha aliyaficha kama chui sikumjua, ubaya umejitoza leo yamenikuta, najuta."

Jamaa alimuamini tu, akijua ni rafiki yake wa kufa na kuzikana, lakini mwenzake alikuwa ni kigeugeu, leo anakuwa mtu na kesho chui.

Ni yale yale tu ya mtu mwema leo, kesho anakuwa mbaya.

Mahasimu wakubwa wa Msondo, DDC Mlimani Park Orchestra wana Sikinde Ngoma ya Ukae, wao wakaja na kibao chao kinaotwa 'Nalala Kwa Tabu.' Ulitoka katikati ya miaka ya 1980, utunzi wake Cosmas Thoboas Chidumule.

"Mwenzenu, usiku huwa silali, nateseka, usingizi kweli sipati nabaki nahangaika. Kuyasema yote ninayoona siwezi, yasije yakaleta, udadisi kwa watu bure. Shahidi yangu ni mama watoto, yeye anajua, kwani huwa ananiona ninavyohangaika.

Nalala kwa tabu mie, yalisema watu lisemwalo kama halipo laja.

Ingekuwa ndoto wala mimi nisingejali, ninawalezea walimwengu muyajue mateso yangu.

Uwaonao wazuri na wabaya ni hao hao. Amini usiamini mimi kuchekea siyo kufurahi nawe kaka."

Maudhui ni yale yale. Mtu akikuchekea siyo kama anafurahi naye, au anakupenda sana. Wakati mwingine 'anacheka jino pembe'.

Huu nao ni msemo unaomtaja mtu ambaye mtafurahi na kucheza naye mdomoni, lakini moyoni ni hasidi, mnafiki na hakupendi.

Hii ndiyo dunia, tujihadhari sana.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HUSNA na mama yake mdogo wakatazamana tena.

"Nadhani itakuwa vizuri zaidi, utakuwa unashuhudia kila kitu. Na utakiri kuwa hakuna nia yoyote ovu, nakuomba sana, kila kitu nitafanya juu yenu."

"Sawa baba, hata mimi nimetafakari naona na mimi nije tu. Kwanza nashukuru kwa sababu umenialika, lakini pia kwa ajili ya usalama na binti yangu na kama kila kitu kitakwenda sawa, kusema kweli litakuwa jambo la kukumbukwa sana." Tabia akasisitiza.

"Ila nachokuomba ni jambo moja."Husna akadakia. "Nini tena shemeji na wewe?"

"Sitaki mazungumzo yoyote ya muafaka na Dan. Akinisalimia na mimi nikamsalimia, hakuna tatizo, lakini sijui tukae tuyasuluhishe, hapana!" Husna akamtahadharisha shemeji yake.

"Na mimi sijawahi kuwa mpatanishi mzuri hata siku moja." Akajibu na kusababisha vicheko.

Yakaendelea mazungumzo ya hapa na pale kiasi kwamba kila mmoja alifurahi. Belo aliaga na hakuwaacha hivi hivi. Akatoa noti mbili shilingi elfu 10 na kumkabidhi shemeji yake huku mama yake mdogo akishuhudia.

"Haya shemeji nakutakia safari njema, nakuahidi tutakuja wote na mama yangu, hatutakuangusha." Husna akamuaga shemeji yake.

Alichotaka Belo kimefanikiwa. Alitaka Dan na Husna wote wahudhurie tafrija yake. Na alikwenda kuwataarifu kila mmoja kivyake.

Hakumwambia Dan kama amemualika mkewe, na wala hakumwambia Husna kama amemwalika ndugu yake. Pamoja na hayo Husna anatambua kuwa Belo na Dan ni ndugu, hivyo si rahisi kwa mumewe kushindwa kwenda kwenye pati ya kaka yake.


Ina maana hapo ni Dan tu ndiye aliyekuwa hajui kuwa mkewe atakuwepo kwenye pati hiyo.

***************************

Hali ya hewa ya Dar es Salaam haikuwa nzuri wala mbaya sana. Kulikuwa na kiwingu ambacho kilifanya kazi ya kuzuia miale ya jua isichomoze na makali.

Kiwingu kilisababisha watu wasiweze kujua muda sahihi hadi waangalie simu au saa kwa sababu ilionekana ni kama saa 12:00 jioni. Ukweli ni kwamba ilikuwa ni saa saba mchana. Kwa hawaida makali ya jua ndiyo yanafanya kazi yake barabara, na joto huwa kali zaidi kiasi kwamba wapo watu wanaotamani hata kujitumbuliza kwenye friji.

Ilionekana pia ni kama mvua itanyesha muda wowote ule. Hata hivyo haikuzuia kuwa siku ambayo ilipangwa kufanyika pati kwa Belo.




Kama ambavyo ilibainishwa huko nyuma, nyumba hiyo ilikuwa ya urithi. Belo, Dan, Tunda na Halima wote walikuwa warithi. Nyumba hiyo ipo Manzese, Tip Top, ambayo ilikuwa ni kubwa na ina vyumba vya uani. Kwa bahati nzuri au mbaya, ni Dan pekee ndiye aliyeondoka nyumbani hapo kwenda kuishi sehemu nyingine. Waliobaki waliendelea kuishi pale kwa sababu ambazo ni familia yenyewe ndiyo inafahamu.

Ilikuwa pia na ukumbi mkubwa ambao ungeweza kufanyiwa vikao. Muda huo ulikuwa umepambwa kwa nakshi mbalimbali, maua, maputo na taa za kumetameta, ikiashiria kuna kitu cha kipekee siku hiyo.

Ndiyo, kulikuwa na pati iliyoandaliwa na Belo. Ilihudhuriwa na watu wengi kidogo, lakini kwa asilimia kubwa ilikuwa ni familia ya kina Belo.

Wengi walikuwa wanajuana. Hata hivyo kuna baadhi ya watu ambao walikuwa hawafahamiani pia. Wengine walishangaa kuwaona wengine wapo na kushindwa kujua ni nani aliyewaalika.

Dan alifika pale mapema, lakini baada ya dakika kadhaa hakuamini macho yake alipomuona mkewe Husna akitinga na mama yake mdogo, Tabia.

Kila akifikiria ni nani aliyemualika kwenye pati hiyo, wala akili yake haikumpa kama itakuwa kaka yake Belo.

"Ataanzaje kwanza kwenda kule. Ataanza kuongea lugha gani ambayo watamsikiliza. Kama mimi ambaye ninafahamika kule nilishindwa ninayefahamika, itakuwa yeye?"

Baadaye akili yake ikamtuma kuwa huenda ni dada zake Tunda na Halima ndiyo walioenda kumualika.

"Mwanamke mwenzake mwanamke, wanaweza kuwa walikutana sokoni, wakasalimiana na kualikana." Akawaza Dan. Wakapata muda wa kusalimiana, lakini hawakuwa na ukaribu, kwani Husna hakuonekana kutaka kuwa karibu na Dan.

Shauku ya Dan ni kutaka kujua mtu ambaye amemualika mkewe Husna. Kufika kwake pale ni jambo lililomuumiza kichwa, lakini kuja nana mama yake mdogo ndiyo kulimshangaza zaidi.

"Ni mtu gani mwenye utaalam wa hali ya juu kuwashawishi hawa wawili kuja kwenye pati ya ndugu yangu wakati mimi mwenyewe walinitoa mbio. Nitaka nimjue nimvishe nishani na ushujaa. Hawa ambao walinipa maneno mpaka nikatoka mbio!" Ajisemea wakati sherehe zikiendelea.

Husna yeye wala hakushishughulisha kutaka kujua nani amemwalika nani. Alijua kuwa wote waliokuwa hapo ni ndugu, jamaa na marafiki, japo wengine naye pia alishangaa anaowajua kuwaona pale. Hakujua kama wana ujamaa, au urafiki na ukoo wa mumewe.

Kitu alichokuwa akitaka kukijua ni kitu kimoja tu. Kumuona mwanamke ambaye ni hawara ya mumewe. Mwanamke ambaye siku ile alimtukana kama atakuwepo. Hakuna na uhakika sana na hilo, lakini katika jicho lake la uandamizi alidhani angeweza kujua na kumuona mtu huyo.

Mara kwa mara alikuwa akimtupia jicho Dan anapotoka kidogo au kurudi ni mwanamke gani anamfuata, au nani anaingia baada ya yeye kurudi ndani.

Akili yake ilimtuma kwa sababu siku ile alijinasibu kuwa familia ya kina Dan inamtambua yeye, basi ni lazima angekuwepo. Na kwa sababu asingeweza kufahamu kama yeye angekuja kwenye pati hiyo, hivyo angefika tu kwa kujipendekeza kwake.

Japo ilikuwa ni pati ndogo tu ya 'bethdei', lakini ilifana. Keki ikakatwa, watu wakaimba. Wakaila. Wakacheza muziki. Wakala na chakula, kunywa na kufurahi.

Wakati ikielekea kwenye kilele ndipo, Belo aliponyanyuka na kuchukua kutoa risala fupi ya shukrani. "Nawashukuru sana wote mlioshiriki kwenye tafrija hii fupi ya 'bethdei' ya binti yangu Tima. Lakini kwa dhati kabisa napenda kumshukuru mke wangu mama Tima ambaye tumeshirikiana naye sana kwenye hili lililotuleta leo hapa. Mwingine ningependa kumshukuru mdogo wangu wa kuzaliwa tumbo moja, Dan. Yeye pamoja na kwamba alipaswa kusafiri leo hii, lakini ameahirisha kwa sababu ya hafla hii.

"Kipekee kabisa kabla sijamaliza ningependa kumshukuru shemeji yangu, Husna na mama yake kwa kukubali ombi langu la kuwaalika na kweli wakatekeleza. Kukubali ni jambo moja, lakini kufika hapa ni jambo lingine. Kusema kweli haikuwa kazi rahisi kuwashawishi kuja kwenye pati hii. Ilikuwa ni jambo la kujitoa muhanga mimi kwenda kwao na kufanya ushawishi kwa ajili ya hili lililotokea.

"Nikisema hivyo nadhani wengi wanajua nini kilitokea huko nyuma, hivyo ilikuwa si rahisi. Lakini walinikaribisha vema kwao, nikafanya nao majadiliano na kuwaalika hapa na ndiyo maana wamefika. Kwao ulikuwa ni mualiko maalum." Belo aliongea. Sauti yake ilipenya vema masikioni mwa ndugu yake Dan.

Ndipo alipofunguka masikio kuwa kumbe kaka yake, Belo ndiye aliyekwenda ukweni kuwaalika mkewe na mama mkwe wake.

"Du! Kaka kaingia kwa gia gani?" Akajiuliza. Baada ya kujiuliza sana akajipa jibu mwenyewe na akili yake ikatulia.

"Husna hakugombana na kaka Belo. Mgomvi wake ni mimi, hivyo asingeweza kumtolea maneno ya shombo na kumtimua. Alikaa, akamsikiliza, wakaelewana." Akajibu. "Ila siwezi kumaliza kufunga tafrija hii bila kumnyanyua rafiki yangu Massawe. Huyu ni rafiki yangu, lakini hatukufahamiana siku nyingi sana, ni muda mfupi tu. Ana machache ya kutaka kuelewa. Karibu sana bwana Massawe."

**ITAENDELEA JUMAPILI**




# Boma yee, Bome Liwanza

JUMAPILI iliyopita asubuhi, mashabiki na wafuatiliaji wa habari za mitandao na Watanzania kwa ujumla walipatwa na mshtuko, zilipotolewa habari za kufariki Mkurugenzi wa Lemutuz TV na blogu ya Lemutuz Brand ambaye jina lake kamili ni William John Malechela.

Alipata umaarufu kutokana na mtandao wake kuwa moja ya majukwaa maarufu kutokana ma maudhui yake na habari mbalimbali za watu maarufu.

Lemutuz, mtu wa mitandao alikuwa na maneno, misemo kauli mbiu mbalimbali maarufu kwenye mitandao ya kijamii kama 'hashtag', ambazo zilizidi kumfanya kuwa maarufu zaidi.

Wakati anaagwa kwenye Ukumbi, gari lililobeba mwili wa marehemu lilipambwa kwa kubandikwa machapisho ya 'hashtag' zake zote, ambapo baadhi walionekana kushangaa na hawakuelewa maana yake.

Nazo ni 'Super Brand', 'Lemutuz', 'Free Education', 'Sweken', 'American Spirit', 'Case Closed', 'Akili Kubwaz', 'Boma Liwanza', 'Boma yee', 'The Big Boss.' Wengi walikuwa wanahitaji japo kwa uchache kuelezwa maana na misemo au 'hashtag' hizo.

Hapa nitaizungumzia ile ya Boma Liwanza na Boma Yee. Hiyo ni bendi ya muziki wa dansi. Inavyoonekana marehemu alikuwa ni shabiki mkubwa wa bendi hiyo ilivyovuma sana na kuwa maarufu Afrika Mashariki.

Bendi ya Boma Liwanza ilianzishwa mwaka 1972 na kuvunjika mwaka 1981 nchini Kenya, ikikusanya wanamuziki wengi kutoka nchini Zaire (Sasa DRC), wakipitia nchi mbalimbali kama Uganda, Tanzania na Zambia kabla ya kufika nchini humo kuweka makazi na kuunda bendi hiyo iliyoondokea kuwa maarufu sana.

Ilikuwa ikirekodi baadhi ya nyimbo zake kwenye lebo ya 'Bana Moja', ambapo wale mashabiki wa muziki wa dansi wa zamani watakumbuka santuri zake zilikuwa na mtu mmoja aliyevaa kofia kubwa aina ya pama.

Boma Liwanza iliyokuwa na kibwagizo kwenye uimbaji wake 'Boma Yee', ilianzishwa na wanamuziki Tabu Fantal, Roy Mosanda, Bibiley Kaba, Christopher Eshu, Nsilu Wabansilu, Etchou Ndjaidi, Lokombe, Loboko Pasi, Jimmy Kasule na wakati mwingine wakiwakodisha Lovy Longomba, Moreno Batamba na Jimmy Monimambo kuwasaidia kuweka sauti wakati wa kurekodi. Baadhi walijiondoa kwenye bendi hiyo na kutengeneza bendi yao waliyoiita 'Special Liwanza.'

Ilikuwa na nyimbo maarufu zilizowateka mashabiki wengi Afrika Mashariki akiwemo Lemutuz, kama, 'Nakoka te', 'Mwana Mobali', 'Lisolo ya Ndako', 'Nirvana', 'Cafe con Leche,''Mbanda Tubi','Biabaza',' Bilobela', 'Mary Akinyi', 'Zala Serieux', 'Ma Bi' na nyinginezo nyingi. Alizikwa Mei 17, kwao Mvumi, Dodoma. Kwaheri, Lemutuz, 'Bome Yee', 'Boma Liwanza.'

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**SPURS YAMTAKA MENDY**
KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kuchukua hatua ya kushangaza kwa kumnunua mlinda lango wa Chelsea raia wa Senegal, Edouard Mendy, mwenye umri wa miaka 31, huku wakitafuta mbadala wa mlinda mlango wa Ufaransa, Hugo Lloris (36), ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. (***Sun***)

**MAGUIRE ANUKIA WEST HAM**
MLINZI wa Manchester United na England, Harry Maguire, anaweza kuhamia West Ham au Tottenham Hotspur huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 akiwa hapendwi tena na kocha, Erik ten Hag. (***Football Transfers)***

**LAMPARD AMTAJA HAALAND**
KOCHA wa muda wa Chelsea, Frank Lampard, amesema alijaribu kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland, katika kipindi chake cha kwanza Stamford Bridge, kabla ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kuhamia Borussia Dortmund. (***Mail***)

**SALIBA AINGIA SOKONI**
WILLIAM Saliba anavutia klabu tatu ambazo hazikutajwa, huku Arsenal ikiiendelea kujadiliana kuhusu mkataba mpya na beki huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22. (***Mirror***)

**SLOT AKARIBIA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur ndio washindani wakuu katika vita ya kumwania kocha wa Feyenoord, Arne Slot, kama mwalimu mpya mwishoni mwa msimu huu. (***Sky Sports)***

**LOFTUS-CHEEK AWINDWA**
KIUNGO wa kati wa Chelsea na England, Ruben Loftus-Cheek (27), anatajwa anajiandaa kuhamia AC Milan, ambao wamemchagua kama kipaumbele cha kwanza wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto. (***Fabrizio Romano)***

**HODGSON SAFI PALACE**
MMILIKI mwenza wa Crystal Palace, Steve Parish, amemmwagia sifa, Roy Hodgson, kabla ya mazungumzo ya mkataba mpya kati ya kocha huyo mkongwe na klabu hiyo. (***Standard***)

**BUTLAND KUHAMIA RANGERS**
GOLIKIPA wa Crystal Palace na England, Jack Butland, mwenye umri wa miaka 30, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Manchester United anakaribia kukubali kuhamia Rangers msimu huu wa joto. (***Mail***)

**JONES NJIA PANDA**
BAADA ya tangazo la kuondoka kwake Manchester United, mlinzi wa England, Phil Jones, mwenye umri wa miaka 31, "anachukua muda" kutafakari hatua yake inayofuata. (***Lancashire Telegraph***)

**ZAHA, FENERBAHCE WATETA**
WAKALA wa mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, mwenye umri wa miaka 30, amekutana na mabosi wa Fenerbahce ya Uturuki na kuchochea tetesi za mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast kuondoka msimu huu. (***Goal***)

**MOURA ATAKIWA MAREKANI**
LUCAS Moura anatathmini chaguo lake baada ya kuamua kuondoka Tottenham Hotspur, huku klabu za Saudi Arabia, Ligi Kuu Marekani na Serie A vikiwa vimewasiliana na mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 30. (***Fabrizio Romano***)

**MOYES APEWA UHURU**
KLABU ya West Ham itamruhusu Kocha, David Moyes, kuamua mustakabali wake ikiwa atawaongoza kutwaa ubingwa wa Kombe la Europa Conference League. (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TEN HAG: RASHFORD HATAONDOKA UNITED

**MANCHESTER,** England

●●● Kocha huyo asema anajiandaa kutia saini mkataba mpya kwa sababu...

MANCHESTER United inaamini mshambuliaji wake, Marcus Rashford, atasaini mkataba mpya katika klabu hiyo, kwa mujibu wa Kocha, Erik ten Hag.

**Rashford ataingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake msimu huu wa joto na ikiwa masharti mapya hayatakubaliwa, mshambuliaji huyo anaweza kuondoka hapo Old Trafford kwa uhamisho huru hapo mwakani.**

Lakini Ten Hag anaamini hilo haliwezekani na ana matumaini mazungumzo yatasababisha mkataba mpya wa muda mrefu.

"Marcus anataka kubaki na tunataka abaki, kwa hiyo nadhani kila kitu kitakuwa sawa," alisema Ten Hag.

United wamefanya maendeleo na baadhi ya mazungumzo ya mkataba na kutangaza mkataba mpya kwa Luke Shaw hapo Aprili, kabla ya beki huyo kuingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake.

Ten Hag amesema anajua ni kwanini klabu hiyo haijafikia makubaliano na Rashford, ambaye amefunga mabao 29 msimu huu, lakini amesisitiza hajali kucheleweshwa kwake.

"Ndiyo, najua kwa nini, lakini sizungumzi kuhusu mchakato huo," aliongeza.

"Acha mchakato uende, kwa mara nyingine, hii sio muhimu kwa sasa kwangu au kwa Rashy, kwake ni kupata mabao mengi zaidi msimu huu na anacheza msimu mzuri na timu inacheza msimu mzuri ili kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuzingatia hilo."

Rashford alikosa mechi ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Wolves kwa sababu ya jeraha na alirejea mazoezini wiki hii.


United wanahitaji ushindi katika mechi mbili kati ya tatu za mwisho ili kumaliza kwenye nafasi nne bora katika Ligi Kuu England na kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
CHELSEA
1 | 1.26
X | 5.28
2 | 9.10

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# LAMPARD ALIKARIBIA KUMSAJILI HAALAND

**LONDON,** England

KOCHA wa muda wa Chelsea, Frank Lampard, amesema "nilijaribu sana" kumsajili, Erling Haaland katika kipindi chake cha kwanza kama kocha pale Stamford Bridge.

Haaland amefurahia msimu mzuri wa kwanza nchini England tangu ajiunge na Manchester City kutoka Borussia Dortmund kwa uhamisho wa euro milioni 60 msimu uliopita, akifunga mabao 52 katika mashindano yote yakiwamo 36 katika mechi 33 za Ligi Kuu England.

City wako ukingoni mwa msimu wa kushinda mataji matatu na wanaweza kutwaa taji lao la tano la Ligi Kuu England katika misimu sita leo kama itashinda dhidi ya Chelsea mechi itakayochezwa kwenye Uwanja wa Etihad.

Lampard anaendelea kuinoa Chelsea kama mlezi kufuatia kutimuliwa kwa Graham Potter mwezi uliopita, na kurejea katika eneo alilotimuliwa awali na klabu hiyo Januari, 2021 baada ya kuiongoza kwa miezi 18.

Mwaka mmoja mapema, katika dirisha la uhamisho la Januari 2020, Haaland alihama kutoka FC Salzburg hadi Dortmund baada ya klabu hiyo ya Ujerumani kuanzisha kifungu cha kutolewa kwa euro milioni 20.

Lampard alifichua alitaka kumleta mshambuliaji huyo wa Norway kwenye Ligi Kuu England kabla ya kuwika na klabu hiyo ya Bundesliga.

"Sijui kama angeamua kuja hapa hata hivyo lakini nilikuwa shabiki mkubwa wa Haaland," alisema Lampard akiuambia mkutano wake na waandishi wa habari jana.

# Hodgson: Zaha atabaki Crystal

**LONDON,** England

ROY Hodgson anahisi nyota, Wilfried Zaha, huenda asicheze tena Crystal Palace msimu huu kwa sababu ya jeraha, lakini anatumaini atachagua kubaki katika klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 alipata tatizo la msuli wa paja wakati wa ushindi wa wiki iliyopita dhidi ya Bournemouth na anatarajiwa kukosa safari ya Fulham na mechi ya mwisho ya kampeni dhidi ya Nottingham Forest itakayofanyika kwenye Uwanja wa Selhurst Park.

Mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast unamalizika msimu wa joto, lakini Palace wanatamani fowadi wao huyo atakubali mkataba mpya, ambao utamfanya alipwe pauni 200,000 kwa wiki.

"Jeraha linaonekana baya zaidi kuliko vile tungependa iwe, kwa hiyo ninahofia hatacheza tena msimu huu - lakini tunaweza tu kutumaini anabaki," alisema Hodgson, ambaye mustakabali wake Selhurst Park unabaki kutokuwa na uhakika hadi mwisho wa kipindi chake cha sasa cha mpito.

"Kuna madaraja mengi tofauti, ni dhiki ifaayo na ikiwa haionekani ndani ya wiki mbili, itachukua muda mrefu zaidi ya hapo, lakini haitaweka mustakabali wake wa muda mrefu hatarini hata kidogo. ."



CHEZA USHINDE KASINO

# WACHEZAJI 3 BLACK SAILOR WAFUNGIWA MIAKA MIWILI

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

WACHEZAJI watatu wa Black Sailor FC wamefungiwa kucheza soka kwa muda wa miaka miwili kutokana na kosa la kumpiga mwamuzi, Ibrahim Ali Ubwa, aliyekuwa anachezesha mechi ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya KMKM, imefahamika.

Mechi hiyo ilivunjika dakika ya 83 baada ya mwamuzi huyo kupigwa baada ya KMKM kupata bao la kusawazisha.

Nyota hao waliofungiwa ni Nassor Hassan, Rajab Abdallah Juma na Yusuph Issa Hassan.

Ofisa Mtendaji wa Bodi ya Ligi Kuu Zanzibar, Hashim Salum, aliliambia Nipashe jana wachezaji hao pia wamepigwa faini ya Sh. 500,000 kila mmoja huku Black Sailor ikipigwa faini ya Sh. milioni 1.5.

"Adhabu hizo zote zimetolewa kwa mujibu wa kanuni ya kuendesha mashindano ya msimu wa 2022/2023 Ibara ya 20(4), bodi pia imewapa KMKM pointi tatu na mabao mawili," alisema Salum.

Aliongeza bodi imetoa onyo kwa timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar kudumisha nidhamu katika kipindi hiki cha lala salama.

Wakati huo huo, Kundemba FC imenusurika kushuka daraja baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Uhamiaji katika mechi ya raundi ya 28 ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa juzi.

Kocha Mkuu wa Kundemba, Ali Vuai Shein, alisema mechi hiyo haikuwa rahisi kutimiza na anawapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kutimiza lengo la kuibakisha timu katika Ligi Kuu Zanzibar.



Wachezaji wa timu za vijana wanaolelewa na Kituo cha Jakaya Kikwete Youth Park wakifanya mazoezi kwenye kituo hicho kilichoko Dar es Salaam ili kujiandaa na mashindano mbalimbali. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Simba, Yanga zatawala tuzo Bara

INATOKA UK. 24

ent Mzize kutoka Yanga (sita) na nyota wa Azam FC, Abdul Suleiman Sopu mwenye magoli matatu.

Kamati hiyo pia imeteua wataowania tuzo ya Kipa Bora wa Ligi Kuu ya Wanwake Tanzania ambao ni Najiath Abbas wa JKT Queens, Winfrida Jedah (Fountain Gate Princess) na Gelwa Yona wa Simba Queens huku tuzo ya mchezaji chipukizi wa ligi hiyo inawaniwa na Winfrida Charles wa Allance Girls, Winfrida Gerald (Fountain Gate Princess) na Jackline Shija wa JKT Queens.

Ally Ally anayewafundisha mabingwa JKT Queens, Juma Hussein wa Fountain Gate Princess na Charles Lukula wa Simba Queens wanawania tuzo ya kocha bora wa Ligi ya Wanawake huku tuzo ya mchezaji bora wa ligi hiyo inawaniwa na Donisya Minja (JKT Queens) na Amina Bilal wa Yanga Princess.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 21/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1658 | Lecce vs Spezia | 2.13 | 3.06 | 3.41 |
| 14:00 | 4330 | AC Ajaccio vs Rennes | 6.39 | 3.89 | 1.48 |
| 15:00 | 5450 | Rayo Vallecano vs Espanyol | 2.15 | 3.30 | 3.10 |
| 15:00 | 5686 | Aalborg vs Midtjylland | 2.79 | 3.40 | 2.37 |
| 15:15 | 4030 | FC Sion vs BSC Young Boys | 5.46 | 4.41 | 1.48 |
| 15:30 | 1391 | PSV Eindhoven vs Heerenveen | 1.23 | 6.03 | 9.24 |
| 15:30 | 2209 | GO Ahead Eagles vs FC Volendam | 1.81 | 3.75 | 3.70 |
| 15:30 | 2434 | Ajax vs Utrecht | 1.24 | 6.00 | 8.60 |
| 15:30 | 2893 | NEC Nijmegen vs AZ Alkmaar | 3.89 | 3.69 | 1.78 |
| 15:30 | 3407 | Rapid Vienna vs LASK Linz | 2.40 | 3.29 | 2.57 |
| 15:30 | 4555 | West Ham vs Leeds | 2.30 | 3.35 | 2.80 |
| 15:30 | 5075 | Waalwick vs Twente | 3.84 | 3.84 | 1.76 |
| 15:30 | 5446 | Emmen vs Feyenoord | 5.80 | 4.70 | 1.42 |
| 16:00 | 1182 | Torino vs Fiorentina | 2.22 | 3.15 | 3.10 |
| 16:00 | 1871 | Brest vs Clermont Foot | 2.02 | 3.39 | 3.34 |
| 16:00 | 2634 | Brighton vs Southampton | 1.21 | 6.19 | 9.98 |
| 16:00 | 4159 | Troyes vs Strasbourg | 5.02 | 4.02 | 1.56 |
| 16:00 | 4737 | Nice vs Toulouse | 1.78 | 3.71 | 3.86 |
| 16:00 | 5074 | Reims vs Angers | 1.38 | 4.70 | 6.59 |
| 16:00 | 5235 | Malmo vs BK Hacken | 1.84 | 3.50 | 3.55 |
| 16:30 | 2412 | Spartak Moscow vs CSKA Moscow | 2.36 | 3.41 | 2.68 |
| 16:30 | 3322 | Mainz vs Stuttgart | 2.39 | 3.40 | 2.65 |
| 17:15 | 5169 | Atletico Madrid vs Osasuna | 1.34 | 4.59 | 7.99 |
| 17:30 | 1630 | FC Basel vs FC Lugano | 2.07 | 3.57 | 3.10 |
| 17:30 | 5893 | FC Zurich vs Grasshoppers | 1.85 | 3.52 | 3.84 |
| 18:00 | 3464 | Lokomotiva Zagreb vs Istra | 2.10 | 3.24 | 3.08 |
| 18:00 | 3600 | Manchester City vs Chelsea | 1.26 | 5.28 | 9.10 |
| 18:00 | 4250 | RB Salzburg vs Sturm Graz | 1.85 | 3.49 | 3.54 |
| 18:05 | 4806 | Lorient vs Lens | 5.00 | 4.10 | 1.55 |
| 18:30 | 1738 | Augsburg vs Borussia Dortmund | 6.24 | 5.03 | 1.37 |
| 18:30 | 3426 | IFK Goteborg vs Hammarby | 2.71 | 3.32 | 2.27 |
| 18:30 | 5245 | Ujpest FC vs Kecskemeti TE | 2.33 | 3.21 | 2.79 |
| 19:00 | 1043 | Copenhagen vs Aarhus | 1.79 | 3.67 | 4.08 |
| 19:00 | 1624 | FC Krasnodar vs Rostov | 2.23 | 3.40 | 2.88 |
| 19:00 | 2304 | Ismaily SC vs Haras EL Hodood | 1.77 | 3.21 | 4.82 |
| 19:00 | 2697 | Apollon Limassol vs Apoel Nicosia | 2.78 | 3.15 | 2.48 |
| 19:00 | 4308 | Napoli vs Inter | 2.75 | 3.20 | 2.41 |
| 19:30 | 2020 | Racing Genk vs Union Saint Gilloise | 2.31 | 3.35 | 2.83 |
| 19:30 | 2887 | Valencia vs Real Madrid | 2.92 | 3.26 | 2.27 |
| 20:00 | 2177 | Casa Pia Atletico vs GD Estoril | 2.11 | 3.27 | 3.27 |
| 20:00 | 4432 | Pacos Ferreira vs Rio Ave | 2.14 | 3.37 | 3.12 |
| 20:30 | 3968 | HNK Rijeka vs Dinamo Zagreb | 2.54 | 3.24 | 2.46 |
| 20:30 | 5959 | Bayer Leverkusen vs Monchengladbach | 1.46 | 4.59 | 5.39 |
| 21:30 | 4866 | Ghazl EL Mahallah vs Pyramids | 6.03 | 3.92 | 1.51 |
| 21:45 | 2472 | AJ Auxerre vs Paris St Germain | 6.54 | 4.58 | 1.39 |
| 21:45 | 4698 | Udinese vs Lazio | 3.49 | 3.34 | 1.98 |
| 22:00 | 1744 | Flamengo vs Corinthians | 1.42 | 4.05 | 6.71 |
| 22:00 | 2690 | Sevilla FC vs Betis | 2.25 | 3.20 | 3.00 |
| 22:15 | 5639 | Valur vs Keflavik IF | 1.31 | 5.18 | 6.83 |
| 22:30 | 4401 | Sporting Lisbon vs Benfica | 2.57 | 3.38 | 2.50 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



UK. 21

**Ten Hag: Rashford hataondoka United**

# Yanga SC, Singida BS hapatoshi FA Cup

## ●●● Makocha watishana haitakuwa mechi rahisi kwa sababu...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi, Yanga kutoka Dar es Salaam wanatarajia kushuka ugenini kuwavaa wenyeji Singida Big Stars katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Liti ulioko mkoani, Singida.

**Mshindi wa mechi ya leo atacheza fainali ya mashindano hayo dhidi ya Azam FC ambayo imetinga hatua hiyo baada ya kuifunga Simba mabao 2-1 katika mchezo wa nusu fainali ya kwanza iliyochezwa Mei 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara.**

Fainali za michuano hiyo ya mwaka huu ambayo bingwa wake anakwenda kuwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika itachezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, aliliambia Nipashe jana, wanakwenda kucheza mechi hiyo kwa tahadhari kubwa kwa sababu Singida Big Stars sio timu ya kubeza.

Kaze alisema Singida Big Stars inaundwa na wachezaji wenye uzoefu lakini ambao hawatakuwa tayari kufungwa mara mbili mfululizo.

Hata hivyo alisema watashuka dimbani hali ya kuwa wachezaji wake hawajapata nafasi ya kupumzika.

"Tunakwenda kwa tahadhari, tunajua umuhimu wa kombe hili, ndiyo maana tumekwenda na kikosi chote, wanachama na mashabiki wajue pamoja na tumecheza mechi Jumatano iliyopita na wachezaji wetu wamekuwa na uchovu, lakini tutapambana kuhakikisha tunashinda mechi hii ili tufike fainali," alisema Kaze.

Naye nahodha wa timu hiyo, Bakari Mwamnyeto, alisema ndoto yao kama wachezaji msimu huu ni kutwaa makombe yote matatu.

"Mchezo utakuwa mgumu kwa sababu hii ni nusu fainali, lakini tumejiandaa vizuri kuwakabili Singida Big Stars kwa sababu tunawajua, tumeshawahi kucheza nao mara kadhaa na tumekuwa tukiwafunga. Benchi la ufundi na wachezaji kwa ujumla lengo na akili yetu ni kupata makombe yote matatu, moja la ubingwa wa Bara tayari, bado la Kombe la FA na Kombe la Shirikisho Afrika," alisema beki huyo.

Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema kila kitu kimekaa sawa na hawaingii uwanjani kwa kuwadharau wapinzani wao kutokana na mafanikio waliyoyapata katika michuano ya kimataifa.

"Lengo tulililoweka ni kutetea kombe letu, hatua hiyo hatutotimiza kama hatutashinda mechi hii. Tunakwenda kucheza na timu yenye ubora, hata ukiangalia matokeo yake kwenye ligi walipo, na hata mchezaji mmoja mmoja wana viwango vikubwa pia, lakini sisi kama mabingwa tunataka kutetea kombe letu," alisema Harrison.

Kocha wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, awali aliipongeza Yanga kwa kufuzu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, lakini akaitahadharisha timu yake haitakuwa mchekea katika mechi hiyo.

Pluijm alisema wamejiandaa kikamilifu na mechi hiyo ambayo kama wakishinda itawapeleka hatua ya fainali ya michuano hiyo ambayo ndio malengo yao yaliyobakia kwa sasa.

"Itakuwa mechi ngumu sana, lakini nina imani, nimewaambia wachezaji wangu wacheze wakiwa na imani watashinda, mimi naitaka hii mechi, tumejifunza makosa ya mechi iliyopita," alisema kocha huyo wa zamani wa Yanga.

Alisema anahitaji wachezaji wake kuonyesha utulivu wanavyokuwa na mpira na hii itawasaidia kutawala mchezo na kupata mabao.



Kiungo wa Simba, Clatous Chama akifanya mazoezi kwa ajili ya kuwakaribisha Polisi Tanzania katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA: SIMBA SC**

## Simba, Yanga zatawala tuzo

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Simba, Yanga na Singida Big Stars wametawala katika vipengele mbalimbali vya kuwania tuzo za msimu huu unaoelekea ukingoni, imefahamika.

Kamati ya Tuzo za Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), jana ilitangaza majina ya wachezaji, makocha na waamuzi, wataowania tuzo mbalimbali za waliofanya vyema katika msimu wa 2022/23, ambazo sherehe zake zitapangwa kufanyika baadaye mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi, tuzo hizo zimegawanyika katika makundi matano ambayo ni ya Ligi Kuu, Kombe la FA, Ligi Kuu ya Wanawake, Utawala na Ligi nyingine zinazosimamiwa na TFF.

Wachezaji watano wameingia katika kinyang'anyiro cha tuzo za Mchezaji Bora ambao ni Mzamiru Yassin wa Simba, Fiston Mayele, Djigui Diarra (Yanga), Saido Ntibanzokiza aliyeichezea Geita Gold na Simba na Bruno Gomes wa Singida Big Stars.

Nafasi ya kipa bora inawaniwa na Aishi Manula wa Simba, Diarra, Benedict Haule wa Singida Big Stars huku tuzo ya beki bora ikiwaniwa na Dickson Job, Bakari Mwamnyeto wote kutoka Yanga, Henock Inonga, Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' wote wa Simba.

Katika michuano ya Kombe la FA wanaowania tuzo za kipa bora ni Haule, Diarra na Abdulai Iddrisu wa Azam FC na inatarajiwa kutangazwa baada ya mechi ya nusu fainali ya pili itakayochezwa leo kati ya Yanga dhidi ya wenyeji Singida Big Stars, kwenye Uwanja wa Liti, Singida.

Wanaowania kiatu cha dhahabu katika mashindano ya Kombe la FA ni Andrew Simchimba wa Ihefu ambaye amefunga mabao saba, Clem-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002